SportPesa
TZS. 619,207,580
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Majaliwa** acharukia wizi nondo ujenzi wa wodi ya kisasa
UKURASA 3



**Pochettino akunwa kiwango cha Neymar**
UKURASA 23


# Nipashe

**Jumanne Oktoba 26, 2021** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580745

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Kesi ya Mbowe kizungumkuti

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**WANAHABARI WASISITIZWA KUHAMASISHA CHANJO YA CORONA**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka wanahabari nchini...

## Vilio miili ya watumishi TANESCO ikiagwa

UKURASA 3



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akiaga miili ya watumishi sita wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) jana, Wilaya ya Mbarali waliofariki kwenye ajali ya gari wakiwa kazini Oktoba 22, mwaka huu, katika Uwanja wa Shule ya Msingi Igawilo jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akionyesha mfano wa hundi ya gawio la Sh. bilioni 12 kutoka Benki ya CRDB kutokana na uwekezaji wa serikali kupitia Mfuko wa Uwekezaji wa DANIDA ikiwa ni sehemu ya gawio la Sh. bilioni 25 lililotolewa kwa serikali na taasisi zake, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB, Dk. Ally Laay (wapili kulia), Mwakilishi wa Msajili wa Hazina, Joseph Mwaisemba (kushoto), Mwakilishi wa Balozi wa Denmark, Oscar Mkude (watatu kulia), Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Neema Mori (wapili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji, Abdulmajid Nsekela (watatu kushoto), na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB, Miranda Naiman. **NA MPIGAPICHA WETU**



# Serikali yapokea gawio la bil. 25/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAGEUKIA WASALITI MECHI CAF** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akimsikiliza mgeni wake Balozi wa Jamhuri ya Kenya nchini, Dan Kazungu EGH, wakati wa mazungumzo alipofika Ikulu jijini Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Kesi ya Mbowe kizungumkuti

**Na Kulwa Mzee**

WAKATI kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) , Freeman Mbowe na wenzake watatu ikitarajiwa kusikilizwa leo, Jaji atakayesikiliza shauri hilo bado kizungumkuti.

Kwa mujibu wa hati ya wito iliyotolewa na kutiwa saini na Naibu Msajili wa mahakama hiyo jana, shauri hilo litaendelea leo, lakini haijajulikana litaendelea mbele ya jaji gani.

Hadi kufikia jana jioni, Nipashe lilimtafuta wakili wa utetezi Peter Kibatala na kumuuliza endapo anafahamu shauri hilo limepangwa kusikilizwa mbele ya jaji gani, alijibu kwamba jina la jaji bado halijajulikana.

Jaji huyo atakuwa ni jaji wa tatu kusikiliza shauri hilo baada ya Jaji Kiongozi, Mustapha Siyani kuanza kusikiliza shauri hilo Septemba 10 mwaka huu, kujitoa Oktoba 20, na jaji wa kwanza, Elinaza Luvanda, kujitoa Septemba 6, mwaka huu ikiwa siku ya saba tangu kuanza kusikiliza shauri hilo Agosti 31, mwaka huu.

Jaji Luvanda alijitoa baada ya Mbowe kuomba ajitoe kwa sababu washtakiwa walikosa imani naye. Leo shahidi wa kwanza Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ramadhan Kingai, anatarajia kuendelea kutoa ushahidi baada ya mahakama hiyo kupokea kielelezo namba moja ambacho ni maelezo ya onyo yaliyotolewa na mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa, maarufu Adamo.

Oktoba 20 mwaka huu, Jaji Kiongozi, Mustapha Siyani aliyekuwa akisikiliza shauri hilo alijitoa kwa sababu ya majukumu aliyonayo, akitoa sababu kwamba itakuwa vigumu kwake kuendelea kusikiliza shauri hilo, ambalo linatakiwa kusikilizwa mfululizo.

Kabla ya kujitoa Jaji Kiongozi Siyani alitupilia mbali mapingamizi mawili yaliyowasilishwa na mawakili wa utetezi baada ya kubaini yanakosa mashiko.

Alitoa uamuzi katika kesi ndogo baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na mashahidi watatu wa upande wa mashtaka na mashahidi watatu wa upande wa utetezi pamoja na majumuisho yaliyowasilishwa na pande zote mbili.

Upande wa utetezi ulikuwa unapinga kupokelewa kwa maelezo ya onyo ya mshtakiwa wa pili Adamu Kasekwa kwa madai yalichukuliwa nje ya muda na kabla na wakati yanachukuliwa mshtakiwa aliteswa.

Jaji Siyani alisema anakubaliana na matakwa ya kisheria kwamba maelezo yanatakiwa kuchukuliwa saa nne tangu mtuhumiwa awekwe chini ya ulinzi, yanapaswa kuanza kuhesabiwa.

Alisema kifungu cha Sheria namba 51 sura ya 20 na kifungu namba 50(2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, muda umeongezwa na unaweza kuongezwa na mkuu wa upelelezi au kwa kuwasilisha maombi mahakamani.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Halfani Bwire, Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Mbowe ambao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo yakula njama kufanya vitendo vya kigaidi Ikiwamo kumdhuru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya Agosti mwaka 2020.

# Serikali yapokea gawio la uwekezaji bil. 25/-

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI jana imepokea gawio la Sh. bilioni 25 linalotokana na uwezekezaji ndani ya Benki ya CRDB.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipokea gawio hilo kwa niaba ya serikali kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay.

Makabidhiano hayo yalifanyika makao makuu ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa taasisi na mashirika ya umma yenye hisa ndani ya benki hiyo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Nchemba aliipongeza benki hiyo kwa kutoa gawio kwa serikali, kwa kupata matokeo mazuri ya fedha mwaka 2020 ambayo yamesababisha kuongezeka kwa gawio kwa wanahisa ikiwamo serikali.

"Ongezeko hili la gawio ni kiashiria tosha kwa serikali kuwa Benki yetu ya CRDB inazidi kuimarika zaidi kutokana na mikakati madhubuti ya kibiashara iliyojiwekea na jambo linalowapa moyo Watanzania na wawekezaji kuwa benki inatoa huduma bora katika jamii," alisema Dk. Nchemba.

Alisema fedha zilizopatikana zitakwenda kusaidia utekelezaji wa miradi ambayo serikali imeainisha katika vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2021/2022 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa 2021/22 - 2025/26 hususan katika sekta ya afya.

"Kipekee kabisa niipongeze Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wote wa Benki ya CRDB kwa kazi nzuri mnayoifanya ambayo imesababisha kupatikana kwa gawio hili nono," alisema Dk. Nchemba.

Kadhalika aliipongeza CRDB kwa matokeo mazuri ya fedha iliyopata katika nusu ya kwanza ya mwaka huu 2021 na faida ya benki imeongezeka kwa asilimia 26 kufikia Sh. bilioni 89 kutoka Sh. bilioni 70.4 zilizoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

"Mkiendelea na kasi hii mwakani tunategemea kupata gawio nono zaidi," alisema Dk. Nchemba.

Alipongeza jitihada mbalimbali za benki hiyo kwa kuchangia maendeleo ya taifa ikiwamo ulipaji wa kodi na kwa mwaka jana ililipa kodi ya Sh. bilioni 181.4. Pia, utoaji wa ajira kwa vijana na uwezeshaji kupitia Sera ya Kusaidia Jamii (CSR Policy). "Nimevutiwa sana na mkakati wa Benki ya CRDB kusaidia kutoa ajira kwa vijana kupitia programu ya mafunzo kazini 'internship' na mafunzo kwa wahitimu 'graduate development program."

Akizungumzia mikakati ya serikali katika kuimarisha sekta ya fedha, Dk. Nchemba alisema mwaka huu, serikali imechukua hatua mbalimbali za kusaidia kuiboresha sekta hiyo ikiwamo kupunguza kiwango cha amana za Benki Benki Kuu, kuanzishwa kwa mfuko wa kukopesha taasisi za fedha, na kupunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kwa ajili ya kutoa mikopo zaidi kwa sekta binafsi.

Kwa upande wake, Balozi wa Denmark nchini, Mette Dissing-Spandet, alisema Denmark inajivunia uwekezaji wake kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania kupitia DANIDA ndani ya benki hiyo. Alisema matokeo mazuri ya kifedha ambayo benki hiyo imekuwa ikiyapata yanaonyesha ni jinsi gani inatoa bidhaa na huduma bunifu na zinazoendana na mahitaji halisi ya wateja.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Laay alisema kuwa gawio ambalo limekabidhiwa jana ni sehemu ya faida ya Sh. bilioni 165.2 baada ya kodi ambayo Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu imeipata katika mwaka wa fedha 2020. Pia ameeleza kuwa benki hiyo itaendelea kutoa huduma bora ili kukidhi mahitaji ya wanahisa wake na wananchi kwa ujumla.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alimhakikishia Dk. Nchemba kuwa benki hiyo kupitia kaulimbiu yake ya "Tupo Tayari" itaendelea kushirikiana na serikali kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha nchini huku akielezea kuwa benki hiyo sasa hivi imejikita zaidi kwenye uwekezaji wa mifumo ya kidijitali ya kutolea huduma kama CRDB Wakala, SimBanking na Internet banking.

Pamoja na kukabidhi gawio kwa Serikali Kuu kupitia mfuko wa uwekezaji wa DANIDA, Benki ya CRDB pia imekabidhi gawio kwa taasisi na mashirika mbalimbali ya serikali ikiwamo PSSSF, NSSF, ZSSF, NHIF, Local Government Loans Board, Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Tumbaku Kanda ya Magharibi (WETCU), Umoja Unit Trust Scheme, TCCIA Investment Company Ltd, pamoja na Halmashauri ya Mbinga, Shinyanga, Mufindi, Chunya na Rungwe.

Serikali ndio mwanahisa mkubwa ndani ya Benki ya CRDB kutokana na kuwa na umiliki wa asilimia 21 kupitia mfuko wa uwekezaji wa DANIDA kushirikiana na Serikali ya Denmark, huku taasisi na mashirika ya umma yakiwa na umiliki wa hisa za asilimia 17.1.

## HABARI KITAIFA

# Vilio, simanzi miili watumishi TANESCO ikiagwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VILIO na simanzi vilitawala jana katika viwanja vya Shule ya Msingi Igawilo jijini Mbeya wakati wa kuaga miili ya watumishi sita wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) Wilaya ya Mbarali, ambao walikufa kwa ajali ya gari wakati wakitekeleza majukumu yao.

Watumishi waliokufa ni Physon Maeda (33), Mwamini Kilumile (26), Prisca Mwalongo (26), Silvano Baraka (27), Samuel Lusingu (31) na Salehe Hamis (36). Majeneza sita yaliyokuwa yamepangwa katika mstari mmoja kwenye viwanja hivyo huku kila jeneza likiwa na picha ya kijana aliyepoteza maisha kwenye ajali hiyo iliyotokea Oktoba 22, yalisababisha baadhi ya watu kushindwa kujizuia na kuanza kububujikwa na machozi.

Aidha, katika zoezi la kuaga miili hiyo, baadhi ya wananchi walijikuta wakiishiwa nguvu na kuanguka, hivyo kulazimika kupata msaada wa kubebwa ili kuondolewa mbele ya majeneza hayo kuruhusu wengine waage.

Baadhi ya ndugu walisikika wakilia, huku wakitaja majina ya marehemu hao na baadhi wakidai kuwa hao wameacha watoto wadogo.

Akiongoza mamia ya wananchi waliofika kuaga miili, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema ofisi yake haiwezi kuvumilia watumishi wa umma waendelee kupoteza maisha kutokana na ajali zinazosababishwa na madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani.

Homera aliliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata madereva wote wa serikali watakaobainika kuvunja sheria za usalama barabarani na kuwaweka mahabusu kabla ya kuwachukulia hatua za kisheria.

"Naliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata madereva wote wa serikali watakaobainika wanaendesha magari vibaya na kuwasweka ndani, hatuwezi kuendelea kupoteza watumishi kwa ajali zinazosababishwa na uzembe wa madereva wetu, tutawanyang'anya hiyo kazi na leseni zao za udereva," alisema Homera.

Alisema katika kipindi cha miezi miwili watumishi wa umma 11 walipoteza maisha kwa ajali za magari ambazo taarifa ya Jeshi la Polisi zinaonyesha chanzo cha ajali hizo ni mwendo kasi.

Agosti 23, mwaka huu, watumishi wengine watano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) walikufa ajalini wakati gari walilokuwa wakilitumia kufukuza gari lingine lililodaiwa kuwa na magendo kugonga gari kwa nyuma wilayani Mbozi mkoani Songwe na kusababisha vifo vyao papo hapo.

Akizungumzia ajali ya gari la TANESCO, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa gari la TANESCO ambalo lilikwepa gari lingine na kupinduka.

"Chanzo cha ajali iliyosababisha vifo vya vijana hawa ni mwendo kasi wa dereva wa gari la TANESCO, akiwa kwenye mtelemko mkali wa Inyala, aliona gari lingine linakuja mbele yake na ndipo akajaribu kukwepa na kuingia korongoni kabla ya kupinduka," alisema Kamanda Matei.

Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, alisema vifo vya vijana hao ni pigo kwa TANESCO na Taifa kwa ujumla, kwa kuwa nguvu kazi iliyokuwa ikitumika kupelekea wananchi umeme imepotea.

Alitoa pole kwa Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO nchini na kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kupoteza nguvu kazi hiyo na kuwaombea marehemu wapumzike kwa amani.


**KUSUDIO LA SCANCEM INTERNATIONAL DA KUNUNUA ASILIMIA 68.33 YA HISA ZA TANGA CEMENT PLC ("TANGA CEMENT"), KAMPUNI ILIYOSAJILIWA NA WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA) KWA NAMBA 5068 NA INAYOENDESHWA KWA MUJIBU WA SHERIA ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Kampuni ya Scancem International DA ("Scancem"), kampuni tanzu ya HeidelbergCement AG ("HeidelbergCement") na Afrisam Mauritius Investment Holdings Limited ("Afrisam") zimeafikiana kwamba Scancem itanunua asilimia 68.33 ya hisa za Tanga Cement ("Ununuzi"). Ununuzi huu utategemea utekelezaji wa au kusamehe kutekeleza, vyovyote inavyofaa, masharti ya msingi ("masharti") ifikapo tarehe 30 Juni 2022 au tarehe nyingineyo itakayokubaliwa na pande zote.

Bila ya kuathiri makubaliano ya mwisho kati ya Scancem and Afrisam ("bei ya ununuzi"), bei ya hisa moja itakayolipwa na Scancem kwa Afrisam ni TZS 3,157 na hivyo kufanya jumla ya fedha itakayolipwa kuwa TZS 137,329 milioni kwa hisa zote, yaani asilimia 68.33, zinazomilikiwa na Afrisam kwenye kampuni ya Tanga Cement. Bei ya ununuzi yaweza kuathiriwa na marekebisho yanayohusu madeni, mtaji wa kufanyia kazi, matumizi mengine na uwezekano wa marekebisho mengine baada ya kufungwa kwa ununuzi. Hivyo basi, ni muhimu kutambua kwamba, kwa sasa hakuna uhakika juu ya bei ya mwisho ya ununuzi wa hisa.

Masharti ya msingi yanayotakiwa kutekelezwa kabla ya kukamilisha ununuzi ni pamoja na; (i) Ruhusa ya Tume ya Ushindani Tanzania ("FCC") kwamba ununuzi umekubaliwa kwa vigezo vinavyokubalika na pande zote, (ii) Ruhusa ya Tume ya Madini Tanzania, ("TMC") kwamba ununuzi umekubaliwa kwa vigezo vinavyokubalika na pande zote, (iii) Ruhusa ya wanahisa wa Tanga Cement juu ya ununuzi kukubaliwa kwa azimio maalum la wanahisa (special resolution) kwenye mkutano maalumu wa wanahisa ulioitishwa kama inavyotakiwa chini ya Kanuni 9(5) ya Kanuni za Ununuzi Mkubwa, Utwaaji na Muunganiko kwenye Masoko ya Mitaji na Dhamana za mwaka 2006 ("Kanuni"), (iv) Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa cheti cha uthibitisho kuwa kodi inayohusiana na ununuzi/uuzaji huu wa hisa imelipwa, (v) Baadhi ya leseni za madini zilizotolewa kihalali au zimeombwa upya na Tanga Cement, (vi) Ruhusa ya Idara ya ufuatiliaji wa fedha ya Benki ya Hifadhi ya Afrika ya Kusini au kama inaruhusiwa, Muuzaji alieruhusiwa, kuhusika na wajibu wa Afrisam (South Africa) Proprietary Limited, ambayo ni kampuni tanzu ya AfriSam Holdings (Pty) Ltd ("AfriSam Group") kama mdhamini kuhusu ununuzi, kutolewa.

Endapo masharti yote yatatekelezwa au yatasamehewa kutekelezwa mapema, basi ununuzi hautakuwa na masharti na hivyo utatekelezwa, ambapo utekelezwaji unatazamiwa kufanyika mapema katika robo ya pili ya mwaka 2022.

Endapo ununuzi utakuwa hauna masharti na ukatekelezwa, utaifanya kampuni ya ScanCem kuwa mmiliki mkubwa wa Tanga Cement. Endapo hili litatokea na kama inavyotakiwa na Kanuni kuu ya pili ya Kanuni tajwa hapo juu, Scancem, baada ya bei ya mwisho ya ununuzi kuwa imeamuliwa, itapeleka ofa ya jumla kwa Tanga Cement ya kutwaa hisa zilizobaki (Ofa ya jumla). Ofa ya jumla inatakiwa kuruhusiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Tanzania ("CMSA"). Ili kuhakikisha kwamba wanahisa wote wa Tanga Cement wanapokea kiasi sawa na bei ya hisa iliyolipwa na Scancem kwa Afrisam kulingana na ununuzi kama inavyotakiwa na Kanuni/sheria, ofa ya jumla itapelekwa tu baada ya kuamua bei ya mwisho itakayolipwa na Scancem kwa Afrisam.

Pande zote mbili zinaendelea kufanya mazungumzo na mamlaka za usimamizi, ikiwemo CMSA, Soko la Hisa la Dar es Salaam ("DSE"), FCC na TMC kuhusu ununuzi huu. Matamko mengine yatafuata kadri mazungumzo yatakavyokuwa yanaendelea.

Wanahisa wa Tanga Cement wanatahadharishwa kwamba hakuna hakikisho kuwa masharti yote yatatekelezwa au kusamehewa kutekelezwa kwa wakati. Hivyo basi, hakuna uhakika kama ofa ya jumla itapelekwa. Wanahisa wanashauriwa kuchukua tahadhari wanapofanya lolote kuhusiana na hisa zao kwenye kampuni ya Tanga Cement mpaka pale tangazo litakapotolewa kuhusu kukamilika kwa ununuzi.

***Kuhusu HeidelbergCement***

HeidelbergCement ni moja ya makampuni makubwa duniani yanayojihusisha na utengenezaji wa vifaa vya ujenzi. Kampuni ni kinara katika soko la uuzaji wa kokoto, saruji na zege iliyochanganywa tayari. Ina wafanyakazi takribani 53,000, katika sehemu zaidi ya 3,000 na kwenye nchi zaidi ya 50. Kampuni ina rekodi ya muda mrefu ya kufanya vizuri kifedha kutokana na utendaji bora wenye uwazi katika kupokea mabadiliko. HeidelbergCement inatambua umuhimu wa uwajibikaji katika kutunza mazingira. Ikiwa kinara wa kupunguza athari za hewa ya ukaa (kaboni), HeidelbergCement inatengeneza vifaa suluhishi katika kudhibiti athari za hewa hiyo katika nyakati zijazo. Nchini Tanzania, HeidelbergCement imekuwepo kwa muda mrefu kupitia kampuni yake tanzu ya Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC), iliyoanzishwa mwaka 1966.

***Kuhusu AfriSam***

AfriSam ni msambazaji mbobezi wa vifaa bora vya ujenzi na mbinu za kiufundi. Vifaa vya ujenzi kama saruji na zege iliyochanganywa tayari (RMC) ya AfriSam imechangia sana kwenye maendeleo ya miundombinu barani Afrika kwa zaidi ya miaka 85. Afrisam iko nchini Tanzania kupitia Kampuni ya Tanga Cement ambayo ni mzalishaji wa saruji ya chapa Simba.

AfriSam
Creating Concrete Possibilities

HEIDELBERGCEMENT

216532802


## PM acharuka wizi nondo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameuagiza uongozi wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Lindi kukamilisha upelelezi na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wote wanaodaiwa kuhusika katika tukio la wizi wa nondo 135 za mradi wa ujenzi wa wodi ya daraja la kwanza, kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, Lindi.

"Watu wote waliohusika na wizi wa nondo za ujenzi wa mradi huu wachukuliwe hatua haraka kwani tusipoanza kuwabana watu leo, wakatambua wajibu wao wa kuwatumikia wananchi miradi mingi ya maendeleo haitakamilika."

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa wodi ya daraja la kwanza katika Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, akiwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani Lindi.

Pia, Waziri Mkuu ameagiza Mganga Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Dk. Charles Mtabo awe makini katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za sekta ya afya wilayani humo, ili kuhakikisha malengo ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu sekta hiyo yanafikiwa.

Kwa upande wake, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, Dk. Ramadhani Maiga, alisema mradi huo unaojengwa kwa awamu mbili unatekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri pamoja na mfuko wa jimbo kwa gharama ya Sh. milioni 184.

Akizungumza na madiwani, watumishi wa umma na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, aliwasisitiza kila mmoja kutambua kwamba yupo wilayani humo, kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na atimize majukumu yake ipasavyo.

# Wanahabari wasisitizwa kuhamasisha chanjo corona

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka wanahabari nchini kuendelea kuwaelimisha Watanzania juu ya umuhimu wa kuchanja chanjo ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Amesema kwa kufanya hivyo, Taifa litakuwa sehemu salama katika maambukizi ya ugonjwa huo sambamba na kupunguza madhara yanayoweza kutokea.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na wahariri na waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali, pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulilenga kutambua mchango wa sekta ya habari katika maendeleo ya nchi, pamoja na kufahamiana.

"Mmekuwa sehemu kubwa katika vita ya kupambana na ugonjwa wa virusi vya corona ulipoingia nchini mwaka 2019 hadi sasa. Hivyo nawaomba muendelee kwa kuwaelimisha Watanzania kuhusu kuchanja chanjo ya ugonjwa huo," alisema Dk.Kijaji na kuongeza:

"Rais Samia Suluhu Hassan ametuletea chanjo, hivyo wanahabari mna wajibu wa kuwahimiza na kuwaelimisha Watanzania juu ya umuhimu wa kuchanja kwa usalama wa Taifa."

**MIAKA 60 YA UHURU**

Dk. Kijaji pia aliwataka wanahabari kushiriki kikamilifu katika maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania yatakayofanyika Desemba 9, mwaka huu, kwamba umoja wa wanahabari ndiyo utawaelimisha Watanzania na nchi jirani kufahamu Tanzania ilivyokuwa, kipi kilikuwapo wakati huo pamoja na changamoto, jitihada zilizofanyika za kufikia uchumi wa kati.

"Sisi (wanahabari) ndiyo tutafanya maadhimisho haya ya miaka 60 ya uhuru yapendeze au yasipendeze kwa kutumia kalamu zetu. Tunapaswa kuionyesha dunia kupitia maadhimisho haya kwamba tulikuwa wapi, tulifanya nini na tunaenda wapi," alisema Dk. Kijaji na kuongeza:

"Tuelezee changamoto tulizopita tangu tulipopata uhuru hadi tulipofikia hapa. Wajibu wetu ni kuelimisha. Ni sherehe ambazo Watanzania ambao hawakuwapo wakati nchi inapata uhuru wanatakiwa kufahamu kilichofanyika."

Kadhalika, Dk. Kijaji alisema wizara yake inatambua changamoto zote zinazoisibu tasnia ya habari na zilizowahi kuwasilishwa kwa Rais Samia, Waziri Mkuu, kwamba zitakwenda kutatuliwa pasipo kumiza mtu yeyote.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, aliwataka waandishi wa habari kufanya kazi kwa misingi ya kitaaluma na weledi.

Balile alisema: "Mkienda kwenye habari mfuate misingi ya kitaaluma, lengo tunataka tuwe na utendaji ulioimarika. Tunataka kuondoka kwenye uandishi usiokuwa wa weledi kwenda kwenye uandishi wa kitaaluma. Tukishindwa kuibadilisha taaluma yetu sisi wenyewe kwa muda huu tusitarajie kama tutaweza baadaye".




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Sekondari Maalum ya Wavulana Nachingwea, jana. Kulia ni Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chingwile na kushoto ni Mkuu wa Wilaya, Hashim Komba. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# TPA yapunguza tozo meli za kusafirisha korosho

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Bandari nchini, Eric Hamis, amesema wamepunguza gharama za tozo kwa asilimia 30 meli zote zitakazofanya kazi ya usafirishaji wa korosho kutoka Bandari ya Mtwara kwa msimu huu wa korosho kwa ajili ya kutoa unafuu kwa wasafirishaji wa zao hilo.

Pia, wamefuta ushuru wa kuhifadhi makontena bandarini kwa msimu mzima wa ununuzi na usafirishaji wa korosho katika bandari hiyo.

Mkurugenzi huyo alitoa kauli hiyo jana mjini hapa baada ya kikao cha pamoja kati yake na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wanunuzi wa zao la korosho pamoja na wasafirishaji wa zao hilo.

Alizitaja tozo zilizopunguzwa kuwa ni punguzo la tozo za Stevedoring kutoka Dola za Marekani 90 hadi 63 kwa kasha la futi 20, kutoka Dola 135 hadi 94.5 kwa kasha la futi 40, sawa na punguzo la asilimia 30.

Punguzo lingine ni pamoja na tozo za Shore handling kutoka dola 90 hadi 63 wa kasha la futi 20 na dola 135 hadi 94.5 kwa kasha la futi 40, sawa na punguzo la asilimia 30.

Katika punguzo hilo, Mkurugenzi alisema kuna punguzo la tozo aridhia kutoka dola 10.552 kwa tani hadi 5.276 sawa na asilimia 0.5 ya mali Pwani (Free On Board).

"Hatutatoza makasha matupu ya kuyahifadhi (storage charges) kwa msimu wa mwaka 2021/22 na hivyo kutoa unafuu wa dola 3.95 kwa siku kwa kasha, huku muda wa makasha yenye mzigo (Loaded/Laden Containers) kukaa bandarini bila tozo ya kuhifadhi itakuwa ni siku 15 hali inayofanya tuwe tumeondoa gharama ya dola 19.8 kwa kila siku inayoongezeka sawa na jumla ya dola 158.4 kwa siku nane," alisema.

Alisema pia Mamlaka ya Bandari imetoa kipaumbele kwa meli zinazotoka Mtwara kuegeshwa Bandari ya Dar es Salaam ndani ya saa 24 na bila gharama hali inayopunguza gharama za uendeshaji kwa wenye meli ambazo zinakadiriwa kuwa kati ya dola 15,000 hadi 30,000 kwa siku.

Awali, Bashe alisema serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa watumiaji wa Bandari ya Mtwara hasa kwa msimu huu wa korosho kwa jili ya kumpunguzia gharama za uendeshaji msafirishaji pamoja na mkulima wa korosho.

Aliongeza kuwa uamuzi wowote unaofanywa na serikali unahakikisha unalinda maslahi ya wakulima, wanunuzi na wasafirishaji.

"Wanunuzi msihofu kushindana kwenye bei ya kununua korosho wala msitoe bei ya chini, shindaneni kwa haki kwa kuwa kila kitu kinaenda sawa na kwa sasa tumeshakuwa na uhakika wa kupata makontena zaidi ya 6,000 yatakayoakuja muda wowote kuanzia sasa," alisema Bashe.

## AZAKI zataja vikwazo ushiriki wa maendeleo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASASI za Kiraia (AZAKI) zimetaja vikwazo kadhaa vitakavyokwamisha wao kushiriki ipasavyo katika kuchangia maendeleo ya nchi.

Miongoni mwa vikwazo hivyo ni Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo inawataka kusajili kila baada ya miaka 10.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari jana kwenye majadiliano ya mchango wa Azaki katika maendeleo ya nchi ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Azaki, Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema sheria hiyo ina vikwazo vingi na suala la kusajili asasi kwa miaka 10 tu linarudisha nyuma maendeleo ya mashirika hayo.

"Kwa mfano Kituo cha Haki za Binadamu ambayo ina miaka 26, sasa hivi inasajiliwa upya, hivyo kwa miaka 10 badala iwe na miaka 36 ni kama inakufa na kuanza upya kwa hiyo juhudi zote za miaka hiyo zinakuwa hazipo tunaona hatukuwapo salama," alisema.

Alisema muda mwingi unatumika kwao kushughulikia masuala ya kiutawala na si kutekeleza miradi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga, alisema suala la usajili, utoaji taarifa na vibali ni kikwazo kwenye utendaji kazi.

"Tulikuwa tunalazimika kupata vibali kwa wizara mbili au tatu kabla ya mradi kutekelezwa kwa hiyo hoja yetu serikali ni moja kwanini tusiweke utaratibu mmoja wa kuwa na dirisha moja kupeleka kila kitu," alisema.

Aliongeza: "Kwenye sheria inayoratibu asasi za kiraia kuna masharti ambayo ni magumu sana kutekelezeka hasa kwa taasisi ndogo ndogo, kwa mfano kuna taasisi ipo Katavi ikipata mkataba inalazimika kuleta Dodoma kwa wizara na hawaruhusiwi kufanya kazi yeyote hadi serikali ipitishe hasa kwa ile inayozidi Sh. milioni 20 ni vyema kuweka utaratibu mzuri ambao si kikwazo."

Alisema katika majadiliano hayo yataibua vikwazo vinavyoonekana kwenye utekelezaji wa sheria na kuwasilisha serikalini.

"Tunatarajia mapendekezo tuliyowasilisha kwa serikali kupitia Waziri wa Afya yatafanyia kazi na kuwa na mazingira wezeshi zaidi ya kufanya kazi kama sekta," alisema.

Alibainisha kuwa katika kikao kazi cha Azaki waliwasilisha maazimio yakufanyiwa kazi kwenye sheria ikiwamo masuala ya kodi kwa asasi hizo.

Alisema kufanya kazi kwa kuaminiana ni jambo la msingi kwa kuwa kunasababisha kutoshirikishana kwenye masuala ya maendeleo.

"Changamoto ambayo tunaiona ni katika kujenga njozi ya pamoja au vipaumbele vya pamoja, tukiweza kufanya hivyo tukaweka kipaumbele kikubwa kimoja na wote tukachangia huko."

## HABARI KITAIFA

# Zitto agonga mwamba dhidi ya Ndugai

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu imetupilia mbali maombi yaliyofunguliwa na Kiongozi wa Chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe dhidi ya Spika wa Bunge, Job Ndugai akidai hana mamlaka kikatiba na kisheria ya kumuita kumuhoji aliyekuwa CAG, Profesa Mussa Assad kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kusema Bunge dhaifu.

Mahakama hiyo mbele ya jopo la majaji watatu, Elinaza Luvanda, Dk. Benhaji Masoud na Yose Mlyambina, limetupilia mbali maombi hayo baada ya kuona hayana msingi na kuamuru kila upande utajilipa gharama zake.

Katika uamuzi wake jopo lilikubaliana na hoja za upande wa serikali zilizowasilishwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata kwamba spika anayo mamlaka kikatiba ya kumuita mtu yeyote kwenye kamati na kwamba CAG katika majukumu yake anapaswa kuwa huru na haki zake zina mipaka.

"CAG ana kinga iwapo angetoa maoni hayo kwamba Bunge dhaifu kwenye ripoti yake inayowasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupelekwa bungeni.

"Wakati anatoa maoni hayo hakukuwa na ripoti yoyote iliyowasilishwa mbele ya Rais iliyokuwa na maoni hayo ya Bunge dhaifu.

"CAG hana kinga ya kuita taasisi nyingine ya serikali dhaifu, mahojiano yalikuwa yanahusu ripoti ya CAG, madai ya udhaifu wa Bunge hayakuwa miongoni mwa maoni yaliyopo katika ripoti yake," lilisema jopo.

Katika shauri hilo Zitto alidai Spika Ndugai hana mamlaka ya kumuita CAG katika kamati, ni kinyume cha sheria na Katiba. Alidai katika kutekeleza majukumu yake ana haki na zinalindwa kikatiba.

Akiwakilishwa na Wakili Jebra Kambole, alidai Spika hana mamlaka ya kumuita CAG katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhoji matamshi aliyotoa kwamba Bunge dhaifu wakati wa mahojiano nchini Marekani Januari 7, 2019.

Alidai baadhi ya watu wana kinga akiwamo CAG, analindwa na Katiba Ibara ya 143(6) na kwamba Mahakama pekee ndiyo yenye mamlaka ya kumuhoji kwa alichofanya na si Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Akijibu, Malata alidai Spika ana mamlaka ya kumuhoji mtu yeyote, CAG alikuwa hafanyi majukumu ya kiofisi alipokuwa akihojiwa na hakuna ripoti iliyowasilishwa kwa Rais ikiwa na mapendekezo kuhusu Bunge dhaifu.

Alidai Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge inatekeleza majukumu ya kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga, maadili na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa kwa Spika.

Alisema kamati itakapojiridhisha kushughulikia jambo husika Mwenyekiti wa kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba kamati imemaliza kujadili jambo husika.

"Kwa mujibu wa kanuni hizo Spika ana mamlaka ya kulipeleka suala lolote au mtu mbele ya kamati," alidai Malata.

# Wazawa walamba ajira maelfu sekta ya madini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Madini imesema katika kutekeleza Sheria ya Madini kuhusu utoaji huruma kibiashara migodini (local content), kumekuwa na ongezeko kubwa la ajira kwa wazawa migodini kwa kipindi cha miezi sita iliyopita.

Imebainisha kuwa kwa kipindi hicho cha kuanzia Aprili hadi Septemba mwaka huu, ajira kwenye sekta hiyo zimefikia asilimia 96 sawa na Watanzania 7,151 kulinganisha na asilimia nne ya wageni sawa na ajira 267 kwenye kampuni kubwa za migodi.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipowasilisha ripoti ya sekta ya madini kwa kipindi cha miezi sita iliyopita kwa wadau kwenye kikao cha Wiki ya Asasi za Kiraia (CSO) mjini Dodoma.

Biteko alisema: "Kati ya kampuni zinazotoa huduma kwenye sekta ya madini, kampuni 961 sawa na asilimia 66 ni kampuni za Kitanzania, wakati kampuni 506, sawa na asilimia 34 ni za kigeni. Kampuni hizi zimeidhinishwa na Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini."

Aliongeza kuwa wizara imeidhinisha huduma za ununuzi zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 579.32, sawa na asilimia 63 ambazo zilifanywa na wazawa kulinganisha na huduma za ununuzi zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 337.19, sawa na asilimia 37 kutoka nchi za kigeni.

Vilevile, Biteko alisema sekta ya madini imeainisha mafanikio makubwa kipindi cha miezi sita iliyopita ikiwamo makusanyo ya mapato, utekelezaji wa sheria ya utoaji huduma (local content) na usafirishaji wa dhahabu.

"Wizara kupitia Tume ya Madini imekusanya jumla ya Sh. bilioni 290.68 kutoka vyanzo mbalimbali ikiwamo mrahaba pamoja na tozo za vibali na ukaguzi na kodi za mwaka.

## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together, we can build a better life)

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021.

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2021 | Robo Mwaka iliopita 31 Juni 2021 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 548.59 | 831.27 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 8,250.04 | 4,832.27 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 33,247.64 | 33,550.32 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 427.88 | 985.74 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 51.11 | 115.78 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 30,126.83 | 36,374.21 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 51,812.46 | 48,480.24 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,242.74 | 1,172.60 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 827.23 | 927.19 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **126,534.53** | **127,269.62** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 31,965.00 | 37,655.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 52,011.51 | 48,469.08 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 Amana Maalumu | - | - |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,119.31 | 1,789.84 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| | 27 Dhima Nyingine | 1,820.83 | 594.11 |
| | 28 Madeni | - | - |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **86,916.65** | **88,508.02** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **39,617.88** | **38,761.60** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 573.03 | 283.58 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 4,222.54 | 4,511.99 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,992.32 | 1,136.03 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **39,617.88** | **38,761.60** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 10,086.28 | 9,890.17 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 1,371.47 | 1,403.76 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 451.87 | 502.62 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 31.31% | 30.46% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.63% | 2.87% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 62.21% | 56.85% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 40.95% | 38.09% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.37% | 93.81% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | -2.49% | 11.29% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | -0.58% | 7.76% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2021 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30 Septemba 2020 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2020 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,484.38 | 2,120.63 | 7,201.42 | 6,325.33 |
| 2 Gharama za Riba | 811.26 | 857.32 | 2,431.70 | 2,428.39 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,673.12** | **1,263.31** | **4,769.72** | **3,896.94** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (50.75) | (8.08) | 87.72 | (60.26) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **230.15** | **110.07** | **575.76** | **449.57** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 32.64 | 39.25 | 97.99 | 135.49 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 197.51 | 70.82 | 477.77 | 314.08 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **827.73** | **864.09** | **2,455.44** | **2,536.78** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 334.90 | 317.93 | 1,034.27 | 963.69 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 9.57 | 8.11 | 21.43 | 17.46 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 483.26 | 538.04 | 1,399.74 | 1,555.63 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,126.29** | **517.38** | **2,802.32** | **1,870.00** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 270.00 | 150.00 | 810.00 | 510.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **856.29** | **367.38** | **1,992.32** | **1,360.00** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 26 | 11 | 61 | 41 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 26 | 11 | 61 | 41 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.73% | 1.24% | 2.17% | 1.63% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 8.71% | 3.96% | 6.88% | 4.94% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 43.49% | 62.92% | 45.93% | 58.36% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.75% | 4.53% | 5.56% | 5.15% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba | Robo Mwaka iliopita 31 Juni 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2021 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30 Septemba 2020 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 856.29 | 538.25 | 1,992.32 | 1,360.00 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | 100.65 | 100.63 | 301.84 | 327.98 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | (3,332.23) | (4,124.54) | (3,387.61) | (9,014.54) |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | (2,147.57) | 8,736.97 | 2,727.61 | 8,831.46 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 890.42 | 281.25 | 1,245.24 | 863.35 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (75.92) | (2,956.99) | (1,082.07) | (1,794.99) |
| Kodi iliyolipwa | (270.00) | (270.00) | (810.00) | (510.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(3,978.36)** | **2,305.56** | **987.32** | **63.25** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | (0.69) | (0.00) | (6.03) | (13.12) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 489.89 | (3,218.91) | (2,171.58) | (4,114.55) |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **489.20** | **(3,218.91)** | **(2,177.61)** | **(4,127.67)** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (64.30) | (123.94) | (188.24) | (189.66) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(64.30)** | **(123.94)** | **(188.24)** | **(189.66)** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (3,553.46) | (1,037.28) | (1,378.53) | (4,254.08) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 39,071.76 | 40,109.04 | 36,896.83 | 48,369.87 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **35,518.30** | **39,071.76** | **35,518.30** | **44,115.79** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 30/09/2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 4,754.21 | 41.35 | - | - | 37,625.56 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,992.32 | - | - | - | 1,992.32 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (531.68) | 531.68 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | 32,830.00 | - | 6,214.85 | 573.03 | - | - | 39,617.88 |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | 32,830.00 | - | 2,308.69 | 828.58 | - | - | 35,967.28 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,658.29 | - | - | - | 1,658.29 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 787.23 | (787.23) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | 32,830.00 | - | 4,754.21 | 41.35 | - | - | 37,625.56 |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2021**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 15-10-2021 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 15-10-2021 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 15-10-2021 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| RAJAB S KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 15-10-2021 |
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 15-10-2021 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 15-10-2021 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

216532602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadau saidieni uchunguzi saratani ufikie wengi zaidi

**JIJINI** Dar es Salaam, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, inashirikiana na wadau mbalimbali kuchunguza maradhi ya saratani, lengo likiwa kuwagundua mapema na kuwasaidia watakaopatikana na matatizo.

Kinachochunguzwa ni saratani ya matiti, tezi dume na shingo ya kizazi. Yote haya ni mambo yanayowaumiza watu wengi, kwavile inaelezwa kuwa wanapofika hospitalini kansa inakuwa imeshafikia kwenye hatua za juu na kuongeza hatari zaidi.

Saratani ni ugonjwa unaoweza kuathiri sehemu yoyote mwilini na chanzo chake kinatajwa kuwa ni uharibifu wa seli pamoja na mifumo inayobeba vinasaba (DNA).

Kwa sababu huathiri nasaba inavuruga mpangilio na mwelekeo wa seli zinazogawanyika bila kufuata taratibu za kimaumbile na mara nyingine hugawanyika kabla hazijakomaa na kusababisha uvimbe kutokana na mrundikano kwenye eneo zilipojikusanya.

Saratani hushambulia viungo vingine vya mwili, huingia kwenye mfumo wa damu na kusafirishwa mwilini kwenda sehemu nyingine hatua inayofanya ugonjwa huo kusambaa na kusababisha kifo.

Wataalamu wanasema ukiwahiwa unatibika na pengine kupunguza athari kwa watu wengi, hivyo tunazipongeza kampeni za kuhamasisha wakazi wa Dar es Salaam na kuwachunguza maradhi hayo.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema kumekuwa na ongezeko la saratani katika miaka ya kuanzia 2000 na kusababisha wengi kuugua na kupoteza maisha.

Ni wazi Tanzania nayo kama ilivyo sehemu nyingine duniani imeathirika na maradhi hayo.

Takwimu za shirika hilo Afrika, zinaeleza kuwa ugonjwa unaoongezeka na kusababisha vifo.

Tanzania nayo tatizo hilo linatishia maisha ya wengi.

Taasisi ya Ocean Road inaeleza kuwa kansa ya mlango wa kizazi ni tishio kwa kinamama, wakati ya matiti nayo imo. Kadhalika ile ya tezi dume nayo inatishia afya ya wanaume wengi.

Hata hivyo, matatizo ya uharibifu wa mazingira yanachochea uwepo wa jua kali na mionzi yake huongeza uwezekano wa kupata saratani ya ngozi, huku kukiwa na maelezo ya ongezeko la saratani ya ini.

Maradhi haya yasiyoambukizwa yanahusishwa na mabadiliko ya mfumo wa maisha kama kula vyakula vinavyokaangwa na vyenye mafuta mengi, kutumia sukari na bidhaa zenye sukari kupindukia, kutofanya mazoezi, unywaji wa pombe kupindukia na kuvuta sigara vyote vikiumiza mwili.

Maisha yanayohusisha kujamiiana na watu wengi yamekuwa chanzo cha ongezeko la maambukizi ya kirusi cha HPV (Human Papilloma Virus) yanayozidisha saratani ya mlango wa kizazi. Ni kwa kuona ukubwa wa tatizo hili kampeni zinafanyika. Ndiyo maana tunapongeza juhudi za kuwaelimisha watu wengi na kuwasaidia kwa kutoa elimu na uchunguzi wa bure mara kwa mara ili waweze kutambua dalili za awali za saratani pamoja na kutibiwa.

Lakini kuwapa elimu ya kurekebisha mfumo wa maisha yao ili kujikinga.

Tunaipongeza serikali kwa vile maradhi ni mengi na huenda saratani haijapewa kipaumbele kikamilifu, kutokana na kuwapo magonjwa mengine ya kuambukiza kama malaria, VVU na UKIMWI, magonjwa ya tumbo lakini Tanzania imekuwa mstari wa mbele kupambana na maradhi hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mnaohusika mjue unyanyapaa huu unawaumiza watoto, taifa

Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya wanafunzi wenye ulemavu mara kwa mara hukumbana na vikwazo kadhaa ukiwamo unyanyapaa unaowakwamisha na kuwakatisha tamaa kuendelea na masomo.

Miongoni mwa wanafunzi wenye ulemavu wanaokumbana na vikwazo kwenye elimu ni wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi, ambao inaelezwa kuwa wanakataliwa na baadhi ya walimu katika shule za serikali. Wanakumbana na tatizo hilo, licha ya serikali kuanzisha utaratibu wa elimu jumuishi ambao unalenga kuwaweka pamoja wenye ulemavu na wazima ndani ya darasa moja.

Mwenyekiti wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHAT), Abdul-Hakim Bayakub, anazungumzia unyanyapaa huo dhidi ya kundi hilo.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Waziri Duniani, jijini Dar es Salaam juzi, anasema chama chao kimefanya utetezi wa elimu jumuishi na mazingira rafiki kwa watoto wenye ulemavu huo, lakini bado kuna vikwazo vya kuwakataa.

Walimu ni walezi wa watoto wote bila kujali ni wazima au ni walemavu, na kama wapo wanaowakataa katika shule wanazosimamia, ipo haja ya kuwaelimisha ili waachane na mienendo hiyo.

Watoto wote wana haki ya kupata elimu, hivyo ingekuwa vyema iwapo ulemavu wao utaheshimiwa ili nao wachangamane na wenzao katika shule jumuishi na kusoma.

Inawezekana mazingira kama hayo ya kuzuiwa yakawafanya baadhi ya wazazi kuacha kuwapeleka watoto wenye ulemavu shuleni, kwa kuhofia kuchekwa, kudharaulika, kushushiwa heshima. Mazingira hayo ya mizengwe, kwa namna moja au nyingine yanaweza kukwamisha lengo la kuwapo elimu jumuishi ambayo ni kuwafanya wanafunzi wote bila kujali ulemavu, wasome pamoja.

Walimu kama walezi, wanapaswa kuwasaidia na kuwa chachu kuondoa vikwazo hivyo ili wanafunzi wenye ulemavu wapate haki ya msingi wakiwa na wenzao wenye viungo kamili.

Lakini, ujumuishaji wa wanafunzi katika elimu mara nyingi unahitaji ushirikiano na taasisi mbalimbali kama za kiafya, kijamii, ustawi wa jamii, maji na usafi wa mazingira, usafiri wa umma na sekta zinazohusiana na haki.

Wadau wakishirikiana kwenye jambo hili, inaweza kusaidia kumaliza vikwazo wanavyokumbana navyo watoto wenye ulemavu hasa wa vichwa vikubwa na mgongo wazi vya kukataliwa kuandikisha shule.

Vilevile, kuna haja ya kuwekeza katika kuongeza ubora wa majengo, vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu ambao serikali imeamua kuwajumuisha na wenzao wazima, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo mwaka huu, anatoa ufafanuzi kuhusu kunyanyapaa watoto wenye ulemavu huo akisema wanatakiwa waendelee kupokelewa shuleni.

Aidha, serikali inaendelea kuboresha miundombinu katika shule zote zinazojumuisha watoto wenye ulemavu.

Anaitaja Sekondari ya Patandi iliyoko Arusha kuwa ni ya mfano kwa kuwa inachukua wanafunzi wote wakiwamo wenye ulemavu, huku ikiwa na walimu wenye utaalamu wa kufundisha wanafunzi wanaoishi na ulemavu.

Kwa hicho alichokisema waziri, kingefaa kuwa mfano wa kuigwa na walimu wengine wa shule za umma zinazoweka vikwazo kwa walemavu waache mtindo huo, ili nao watimize ndoto zao kwenye elimu.

Viongozi wa ASBAHAT wanabainisha kuwa wapo wenye ulemavu huo ambao wamesoma na kuhitimu masomo na sasa wanategemewa katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi katika utaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

HABARI KITAIFA

# RC awataka watemi kukemea fikra potofu

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, amewataka watemi wote mkoani humo kukemea fikra potofu na kuenzi mila na tamaduni zilizopo, ili kuongeza amani kwenye mkoa na kuwezesha wananchi kuishi kwa utulivu.

Akizungumza na watemi kutoka katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo, alisema wanapokuwapo wazee wanaokemea matendo yasiyofaa katika jamii, vijana wanaogopa kufanya maovu.

Alisema ili kuhakikisha watemi wanasikilizwa shida zao na kupata nafasi ya kutoa ushauri wa viongozi na watendaji wa serikali, ataawaandikia barua wakuu wote wa wilaya katika mkoa huo, ili wawatambue watemi hao.

"Mkemee mambo maovu, kama huko mlipo mkiona kuna kitu hakiendi vizuri mkikemee maana tunataka maendeleo tukimbie, sasa hivi mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameleta fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika mkoa wetu kwa kila wilaya, tunataka amani, ili kuwaletea wananchi maendeleo endelevu," alisema.

Aliwahimiza wananchi wote ambao hawajachanjwa chanjo ya UVIKO-19, kujitokeza kwa kuwa mkoa umepokea dozi nyingine za chanjo hiyo.

"Wazee wangu kama bado hamjapata chanjo ya UVIKO-19 sasa imeletwa dozi nyingine, tuliletewa ya awali dozi 45,000 tukachanja wananchi ikaisha na sasa tumeletewa tena dozi 61,190 na tayari zimekwisha sambazwa katika wilaya zetu zote, wananchi mjitokeze mchanje," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Watemi mkoani humo, Hermes Nyarubamba, alisema utemi ulipotea, lakini sasa wameona ni vyema kuurudisha na wameunda umoja wao, ili kuhakikisha mema yote yanaenziwa kwa manufaa ya Wanakagera.

"Usipojua asili yako ni kama mtumwa, kwa maana utaishi maisha ambayo hujui na kila kitu utakacholetewa utakifuata, wakati sisi tuna utaratibu wetu, tuna mila na desturi zetu lazima tuzienzi," alisema Mtemi Nyarubamba..

# Serikali kuongeza hadhi soko madini mkoani Dar

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla amesema serikali imedhamiria kukuza na kuboresha soko la madini mkoani humo kwa kulifanya kuwa la kisasa zaidi ili kuvutia wateja wa ndani na nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha wadau wa madini na kwamba uboreshaji wa soko hilo utaiwezesha serikali kupata kodi pamoja na kuwanufaisha wafanyabiashara kwa ujumla.

Alisema Mkoa wa Dar es Salaam una kila sababu ya kuwa na soko kubwa la madini kama ilivyo Dubai ili lisaidie kuinua pato la nchi na kuinua kipato cha wadau mbalimbali wanaojihusisha na biashara hiyo katika mkoa huo na taifa.

"Tangu kuanzishwa kwa soko la madini mkoani Dar es Salaam, biashara zenye thamani ya Sh. bilioni 23.6 zimefanyika na kuwezesha serikali kupata kodi isiyopungua Sh. bilioni 1.6," alisema Makalla.

Kadhalika, alisema uwapo wa soko hilo mkoani hapo umesaidia kupungua kwa vitendo vya wizi na utapeli wa madini jambo ambalo limesaidia kuchochea kuongezeka imani kwa wanunuzi wa madini wa ndani na nje ya nchi.

Aidha, aliwaelekeza wote waliopewa vibali vya kuchimba mchanga, vifusi na kokoto katika mkoa huo kufanya jukumu hilo kwa kufuata sheria na miongozo ikiwa ni pamoja na kushirikisha wakazi wa eneo husika.

Aliahidi kwa kushirikiana na wizara husika kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara wa madini katika mkoa huo, ili kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji biashara utakaokuwa na tija kwao na kwa taifa kwa ujumla.




Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa Vodacom Tanzania, Rosallyn Mworia (katikati), akipokea tuzo kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula, katika mkutano mkuu wa TEHAMA uliofanyika jijini Arusha mwishoni wa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ruvuma kinara chanjo ya UVIKO-19

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKOA wa Ruvuma umeongoza kitaifa katika utoaji chanjo ya UVIKO-19 kwa kutoa chanjo kwa watu 44,549 sawa na asilimia 148.5.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, alipokuwa akifungua kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mpango wa jamii shirikishi na harakishi wa utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 kilichofanyika Manispaa ya Songea.

"Nitumie nafasi hii kupongeza wanaRuvuma kwa mwitikio mkubwa ambao kwa hakika umesababisha mkoa wetu uongoze kitaifa," alisema Brigedia Jenerali Ibuge.

Alisema Mkoa wa Ruvuma ulianza rasmi utekelezaji wa chanjo kwa wananchi Septemba 22 hadi Oktoba 14, mwaka huu na kwamba ulivuka malengo kwa kumaliza dozi 30,000 ulizopewa kwa awamu ya kwanza na kuongeza dozi nyingine za ziada 14,000, hivyo kufikia dozi zaidi ya 44,000.

Hata hivyo, alisema serikali ya Tanzania imepokea dozi zaidi ya milioni moja za chanjo ya UVIKO-19 aina ya Sinopharm kwa ajili ya kuendelea kuwapatia wananchi wake chanjo, ambapo Mkoa wa Ruvuma umeletewa dozi zaidi ya 31,000 ambazo zilitarajiwa kuanza kutolewa kwa wananchi jana. Amewaagiza watendaji wa halmashauri zote mkoani Ruvuma kuhakikisha wanasambaza chanjo haraka katika vituo vyote 298 vinavyotoa chanjo, na kwamba wataalamu wa afya watoe elimu ya chanjo ya Sinopharm ili ifahamike vizuri kwa wananchi kabla ya kuamua kuchanja kwa hiari.

Mratibu wa chanjo Mkoa wa Ruvuma, Winbroad Mvile, alitaja chanjo ya Sinopharm kuwa inatolewa mara mbili ili kukamilisha dozi, na kwamba chanjo hiyo inatengeneza kinga dhidi ya UVIKO-19 kwa asilimia 95.

Alisema mkoa umeletewa dozi zaidi ya 31,291 za Sinopharm ambapo Manispaa ya Songea imepewa dozi 5,300, Tunduru 5,300, Namtumbo 5,300, Halmashauri ya Mbinga 3,572, Nyasa 3,572, Halmashauri ya Songea 3,572, Mbinga Mji 3,572 na Madaba 1,103.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Jairy Kanga, aliwataka wananchi ambao hawakupata chanjo katika awamu ya kwanza kujitokeza ili Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla kufikia hatua ya kupata kinga kundi kufikia asilimia 60 hadi 70 ya watu wawe wamepata chanjo.

# Wahamasishwa kunywa dawa kujikinga minyoo, mabusha

**Na Shufaa Lyimo**

WANANCHI wametakiwa kujitokeza kunywa dawa zinazotolewa kuzuia ugonjwa wa matende, mabusha pamoja na minyoo kwa watoto na watu wazima.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mganga Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alisema dawa hizo zina faida kubwa kwenye mwili wa binadamu na kuwataka wananchi wasizipuuzie, hasa ikizingatiwa ni dawa ambazo serikali imeamua kuzitoa bure ili kila mwananchi apate kinga.

"Ninaomba wananchi wajitokeze kwa wingi kunywa dawa ambazo zinatolewa na wauguzi wetu wa afya kutoka vituo mbalimbali dawa hizo zina faida kubwa ndani ya mwili wa binadamu kwa sababu ukiangalia minyoo inasababisha mtu kupata matende hakuna asiyefahamu adha ya ugonjwa wa matende," alisema Mfaume.

Pia, alisema ugonjwa wa mabusha unapompata mtu huwa unampa wakati mgumu na wakati mwingine ajione kama jamii inamnyooshea vidole na anapojikinga mapema ni vigumu kupata tatizo hilo kiurahisi.

"Kuna minyoo ya tumbo hiyo ni hatari sana katika mwili wa binadamu wakati mwingine inaweza kukusababishia kuwa na upungufu wa damu, hivyo nishauri wananchi wasisite kuzitumia dawa hizo," alisema.

Alisema utoaji dawa ulianza Oktoba 24 na walengwa ni watoto wenye umri kuanzia miaka mitano na kuendelea.

Hata hivyo, alisema haziruhusiwi kutumiwa na wanawake wajawazito na kwamba dawa hizo zimefanyiwa utafiti wa hali ya juu na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Kata ya Msimbazi Magharibi, Ally Mtakuja, aliwashukuru wananchi wake kutokana na kujitokeza kwa wingi na kuwaondoa hofu baadhi ya wanaofikiri zitawaletea madhara kiafya.

"Tangu zoezi lilipoanza jana (Jumapili), wananchi wamejitokeza kwa wingi kunywa dawa hizi kiujumla zoezi linaendelea vizuri na linaendelea mpaka Ijumaa," alisema Mtakuja.



Mlezi wa Jumuiya ya Wanafunzi wa UKWATA na CASFETA, Noah Kadiva, akitoa cheti kwa mmoja wa wahitimu wa kidato cha nne kutoka Shule ya Sekondari ya Salma Kikwete mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam. **PICHA: ANAELI MBISE**

# PRST yabaini vikwazo upatikanaji wa habari

**Na Halfani Chusi**

CHAMA cha Maofisa Uhusiano kwa Umma (PRST), kimebaini uwapo wa vikwazo mbalimbali katika upatikanaji wa taarifa kwa wanahabari kutoka kwa baadhi ya maofisa uhusiano katika taasisi za umma.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Mtendaji wa Chama cha Maofisa Uhusiano kwa Umma, Ndege Makula, wakati alipokuwa akiongea na waandishi wa habari kuelekea mkutano mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 28-29 uliolenga kujadili masuala mbalimbali, ikiwamo vikwazo vinavyowakumba waandishi wa habari wakati wakitimiza majukumu yao.

Alisema walibaini uwapo wa vikwazo hivyo baada ya kutembelea vituo mbalimbali vya habari na kufanya mahojiano na waandishi na kubainisha kuwapo kwa hali hiyo.

"Kuna matatizo yanayowakabili waandishi wa habari ambayo yanasababishwa na maofisa habari wa umma, pia na maofisa habari nao watapata nafasi ya kuwasilisha kero zao kwa hiyo huu ni mkutano wa kwanza ambao umelenga zaidi kwenda kujadili namna ya kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji kazi kati wa waandishi wa habari na maofisa uhusiano kwa umma.

Kwa upande wake Rais wa chama hicho, Loth Makuza, aliwataka wadau wanaohusika na masuala ya taaluma ya habari kuhudhuria kwa wingi katika mkutano huo.

**Alisema walibaini uwapo wa vikwazo hivyo baada ya kutembelea vituo mbalimbali vya habari na kufanya mahojiano na waandishi na kubainisha kuwapo kwa hali hiyo.**

# Serikali yaweka mikakati huduma bora afya

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeagiza vituo vya afya na hospitali za rufani nchini kuweka mpango mkakati wa kutoa huduma bora za afya kwa wateja wao baada ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Mpango wa Taifa wa Bima ya Afya, ili kuondoa malalamiko.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, wakati akifungua mafunzo ya huduma bora kwa wateja yaliyoandaliwa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Mloganzila yanayofanyika mjini hapa.

Dk. Gwajima alisema, suala la kutoa huduma bora kwa wateja kwa sasa sio hiari bali ni lazima kutokana na mabadiliko ya mifumo mbalimbali ambayo tayari serikali ilishazindua mpango huo tangu mwaka 2000 na baadaye kurudiwa tena.

Alisema katika kuhakikisha mpango huo unapata mafanikio yaliyokusudiwa ni lazima kuwapo na ajenda ya kuzungumzia mikataba ya wateja kwa kila hospitali nchini.

Alisema utekelezaji wa mikataba hiyo kwa kila hospitali utaleta matunda kwa taasisi husika kujitangaza vyema kwa wateja na kukimbiliwa na kila mtu kwa ajili ya kujipatia huduma bora, hatua ambayo itaongeza mapato yake.

"Huduma bora kwa mteja ni suala mtambuka, hivyo endapo huduma zikitolewa kwa ubora hii itasaidia hospitali husika kujitangaza vyema kwa wateja pamoja na watoa huduma kujiwekea kama mtaji wa kukimbiliwa na wateja hivyo ni lazima sasa tubadilike hasa wakati huu wa kila mwananchi anatakiwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Profesa Lawrence Museru, alisema wamepewa dhamana ya kuhakikisha hospitali zote nchini zinatoa huduma bora kwa wateja wao na zipo baadhi zimekuwa zikikiuka.

Profesa Musere alisema kutokana na ukiukaji huo wameamua kutoa mafunzo hayo na kwa kuanzia tayari watumishi 2,000 kati ya 3,300 wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Mloganzila wameshapatiwa mafunzo hayo ya kutoa huduma bora kwa wateja.

Alisema baada ya mafunzo hayo wameamua kutoka nje na kutoa mafunzo hayo kwa watumishi wa hospitali zote nchini na yatakuwa endelevu, ili kuhakikisha wateja wa huduma za afya wanapatiwa huduma bora na kwa wakati.

Mafunzo hayo yanashirikisha Taasisi ya Tiba ya Mifupa,Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Mirembe, Hospitali ya Kanda ya Bugando, Hospitali za Rufani, Hospitali za Taasisi za Kidini, Vyuo vya Mafunzo ya Afya, Baraza la Madaktari waTanganyika, Baraza la Wauguzi na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pamoja na taasisi nyingine zinazohusiana na afya.

## HABARI KITAIFA

# Agizo h/shauri kuwatambua watoto wote wenye ulemavu

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeziagiza halmashauri zote nchini kuwatambua watoto wote wenye ulemavu na kubainisha matatizo ya ulemavu wao na kubainisha huduma zinazohitajika kwa kila mtoto.

Halmashauri pia zimetakiwa kuhakikisha zinatekeleza matakwa ya sheria ya watu wenye ulemavu kwa kuweka rejista ya watu wenye ulemavu na kuihuisha mara kwa mara.

Maagizo hayo yalitolewa jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, kwenye maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi duani.

Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Chama cha Wazazi Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT) na kufanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Waziri Ummy aliwakilishwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, pia alizitaka halmashauri kuvitambua vituo vyote vinavyolea na kutoa huduma za marekebisho kwa watoto wenye ulemavu huo na kuwasilisha taarifa katika mamlaka husika.

Mbali na hayo, aliziagiza kubuni programu za kuzisaidia familia zinazolea watoto wenye ulemavu wakiwamo wazazi wa watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi, hasa kuimarisha uchumi wa kaya na huduma za msaada wa kijamii na kisaikolojia.

"Pamoja na hayo, wazazi wote wa watoto wenye ulemavu washiriki ipasavyo kuwalea watoto hao na kuepuka kukwepa majukumu kwa kuwatelekeza watoto," alisema Ummy.

Aidha, alisema, upatikanaji wa bima ya afya ni muhimu kwa watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, lakini akafafanua kuwa kumekuwapo na changamoto katika eneo hilo.

"Suala hili linahitaji kufanyiwa ufuatiliaji wa karibu na majadiliano ya pamoja na wadau mbalimbali wa masuala ya bima, wizara yangu itaratibu suala hili kwa ukaribu kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa kile ambacho kinaweza kukwamisha upatikanaji wa bima hiyo," alisema.

Awali akisoma risala, Mwenyekiti wa ASBAHT Taifa, Abdul-Hakim Bayakub, aliiomba serikali kufanya marekebisho kwenye sera ya matibabu bure kwa watoto chini ya miaka mitano ili wapatiwe bima ya afya itakayodumu kwa miaka mitano tangu wanazaliwa.

"Pamoja na matibabu, watoto wenye ulemavu huu hawakubaliki maeneo mengi. Mfano sheria ya bima ya afya, kupata bima ni kabla ya kuugua, lakini watoto hawa wanazaliwa na ulemavu na anaonekana ni wagonjwa, wanatumia gharama kubwa, " alisema Bayakub.

Alisema ni vyema mashirika ya bima yakatambua kuwa, huo ni ulemavu wa kuzaliwa nao na siyo ugonjwa.

Akifafanua kuhusu gharama za vipimo na matibabu ziko juu hali inayosababisha baadhi ya wazazi kukata tamaa kwa kwa kukosa uwezo.

"Gharama za upasuaji kichwa kikubwa ni Sh. milioni 1.3, mgongo wazi ni Sh. milioni 1.6, kama mtoto ana matatizo yote mawili, gharama yake ni Sh. milioni 1.8, vipimo vya CT Scan ni Sh. 250,000 na MRI ni Sh. 450,000," alisema.

Daktari Bingwa wa mishipa na fahamu wa Taasisi ya Mifupa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MOI), Dk. Hamis Shaban, alisema, taasisi hiyo imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na ASBAHT, ili kuhakikisha wanasikia maisha ya watoto wenye ulemavu huo.

Wito wangu ni kwa wazazi kutowaficha watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi wazi wakiamini kuwa ni laana, uchawi au jambo lingine," alisema Dk. Shaban.

Alisema, ni muhimu kumuwahisha mtoto hospitalini pale mzazi anapoona dalili za ulemavu huo kwa mtoto wake badala ya kwenda kuamini mambo ambayo hayapo.

## Waziri awataka vibarua, mafundi bandarini uzalendo

**Na Gurian Adolf,** NKASI

SERIKALI imewataka mafundi, na vibarua ambao ni wazawa wanaoendelea na kazi za ujenzi katika miradi ya bandari iliyopo mkoani Rukwa kuwa wazalendo wanapofanya kazi zao.

Imesema hatua hiyo inatokana na miradi inayotekelezwa katika maeneo hayo ina tija kwao na vizazi vyao.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo jana wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa Bandari ya Kasanga iliyopo Wilaya ya Kalambo mkoani humo.

Aliwataka Watanzania walioajiriwa katika miradi hiyo pamoja na vibarua kuwa wazalendo kwa kutofanya hujuma zozote ikiwamo kuiba vifaa vya ujenzi, kwani miradi hiyo ni yakwao na wao na vizazi vyao ndio wanufaika wakubwa.

Waitara alisema kuwa pamoja na kuendelea kwa ujenzi wa bandari za Kasanga, Kipili na Kabwe iliyopo mkoani Rukwa pia zipo meli zinazotokea nchi jirani kwa ajili ya kupakia mizigo, hivyo wapo wageni ambao ni wafanyakazi wa meli hizo, wawe wanawachunguza nyendo zao na kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama.

"Naomba niwasihi sana wote mnaofanya kazi hapa, kuweni makini na hawa wageni waofika kuchukua mizigo yao... tunahitaji usalama wa nchi yetu, msiwaamini tu, toeni taarifa kwa mamlaka husika ili zichukue hatua kuweni wazalendo na nchi yenu," alisema.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, Aida Keenan, aliiomba serikali kuzijenga barabara zinazoelekea katika bandari za Kipili na Kabwe kwa kiwango cha lami ili zipitike kipindi chote cha mwaka kwa kuwa ndizo zinatumika kupitishia mizigo kwenda bandarini ili kusafirishwa nchi jirani.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, akiongea na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) waliomtembelea ofisini kwake kwa ajili ya kuanza kampeni ya utoaji elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango mkoani Rukwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka somo la kilimo hai ngazi ya chini

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imeshauriwa kuanzisha mitaala ya somo la kilimo hai kuanzia ngazi ya chini ya elimu ili kujenga uwelewa kwa jamii juu ya umuhimu wa kilimo hicho kwa mustakabali wa taifa.

Ushauri huo umetolewa na wadau mbalimbali wa kilimo waliohudhurka kongamano la pili la Kitaifa lililofanyika jijini Dodoma Oktoba 21-22.

Mmoja wa wadau hao, Richard Mhina, Mkurugenzi wa Taasisi inayojishughulisha na utoaji elimu kwa wakulima na kuwawezesha ya Floresta Tanzania yenye makao yake makuu mkoani Kilimanjaro, Richard Mhina, alisema kwa sasa masuala ya elimu yanafundishwa na kusoma kuanzia ngazi za juu ya elimu ikiwamo vyuo vikuu na taasisi kubwa za elimu kitu ambacho kinapunguza uwelewa wa masuala ya kilimo kwa jamii kubwa ya wakulima.

Alisema Floresta imeandaa vitabu vya elimu kwa ajili ya wakulima kupata elimu, lakini bado jitihada za serikali zinahitajika na wao Floresta wapo tayari kushirikiana na serikali katika kutoa elimu ya kilimo kwa jamii na shuleni.

"Serikali isione ni ziada kufundisha somo la kilimo hai, bali elimu hii inatakiwa kuanza kutolewa kwa vijana shuleni. Kwa upande wetu tunatoa elimu kwa wakulima, lakini tumeandaa vitabu kwa ajili ya vijana na tupo tayari kushirikiana na serikali," alisema Mhina.

Alisema kwa sasa taasisi yake imewafikia wakulima 11,000 wakiwapa elimu na kuwawezesha kwenye kilimo.

Alisema wanashirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) pamoja na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela kutoa elimu na mafunzo kwa wakulima.

Kwa upande wake mdau wa kilimo ambaye ni Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, alisema ni vyema elimu ya kilimo hai ukaanza kutokewa shuleni ili kuiponya ardhi na jamii ya Tanzania.

# Mpango wa maendeleo wa Waislamu Pwani waanza

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amezindua mpango mkakati wa maendeleo wa miaka mitano wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Pwani unaotarajiwa kugharimu shilingi bilioni 43.

Mpango huo ulizinduliwa mwishoni mwa wiki wakati wa mkesha wa Maulid uliofanyika Mailimoja Wilaya ya Kibaha.

Ulega aliupongeza mkakati mpango huo na kusisitiza kuheshimiana, kushirikiana na kufungua milango ya wahisani katika utekelezaji wa mipango yao.

Mufti wa Tanzania, Abubakari Zuberi, aliupongeza mpango huo na kusema kwamba utakapokamilika utaleta mabadiliko ya uchumi kimaendeleo kwa BAKWATA mkoa wa Pwani na kwamba viongozi kuusimamia ukamilike kwa wakati. Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu kusimamia haki pamoja na kuelimishana katika utaratibu wa kueleweshana.

Alisisitiza kumaliza tofauti kwa kukutana badala ya kutumia njia nyingine ambazo zinaweza zisitumike vizuri kuilinda amani.

Kunenge alipongeza mpango huo ambao unaenda kutoua huduma muhimu kwenye jamii na kutumika kuleta maendeleo.

Shekhe wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, alielezea kuwa katika mpango huo wanatarajia kujenga zahanati vyuo vya ufundi (VETA) na kituo maalumu kwa wanafunzi wenye vipaji maalumu.




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (kulia), akikabidhiwa madawati 100 na Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield, kwa ajili ya Shule ya Sekondari Kijitonyama, mkoani Dar es Salaam. Sherehe hiyo ilifuatiwa na upandaji miti, ikiwa ni sehemu ya kampeni ambayo inataka kurejesha mfumo wa ikolojia kwa kupanda mti kwa kila dawati linalotolewa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yawezesha shule kupatiwa taulo za kike

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

JUMUIYA ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, imeishukuru kampuni ya ukandarasi ya Ovans Construction LTD kwa kutoa msaada wa taulo za kike zenye thamani zaidi ya Sh. milioni mbili kwa wanafunzi wa shule za sekondari Mkinga na ya wasichana ya Mbinga, kuwapunguzia adha wanapokuwa na uhitaji wa taulo hizo.

Aliyetoa pongezi hizo ni Katibu wa Jumuiya hiyo, Angelo Madundo, wakati wa kugawa taulo hizo kwa wanafunzi wa shule hizo, ambapo Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mbinga imepata taulo 932 na Sekondari ya Mkinga taulo zaidi ya 300, alisema kuwa Kampuni ya Ovans Construction Ltd, ilipokea ombi kutoka kwenye Jumuiya ya Wazazi wa CCM Wilaya ya Mbinga juu ya uhitaji wa taulo za kike kwa wanafunzi na kampeni hiyo ikakubali kutoa msaada huo.

Madundo alisema kuwa Jumuiya ya Wazazi baada ya kufanya utafiti juu ya baadhi ya wanafunzi wa kike kutokufanya vizuri kwenye masomo yao, ilibainika ni kutokana na baadhi ya changamoto ikiwamo ya kukosa taulo hizo.

"Kwa moyo wa dhati Jumuiya ya Wazazi tunaishukuru kampuni hiyo ambayo inaongozwa na mkurugenzi wake Valence Urio kwa msaada huo, ambao utawafanya watoto wetu wanafunzi wa kike kumpunguza changamoto ya uhitaji wa taulo hizo," alisema Madundo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mbinga, Efigenia Nzota aliishukuru jumuiya hiyo kwa kutambua changamoto za wanafunzi hao na kuwa msaada huo utawafanya wanafunzi kuhudhuria masomo yao kikamilifu. Nzota pia ameipongeza serikali kwa kutoa fedha za kuboreshea miundombinu mbalimbali ikiwamo ya shule na kuzifanya shule hizo ziendelee kuwa katika mazingira rafiki ya kusomea.

Naye mwanafunzi wa kidato cha nne katika Sekondari ya Mkinga, Desidelia Chazi, akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, alisema kuwa wanafunzi wa kike wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya taulo hizo sasa changamoto hiyo itapungua, huku akiishukuru Jumuiya ya Wazazi ambayo ndiyo inayomiliki Shule ya Sekondari ya Mkinga ambayo inawanafunzi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita na ina wanafunzi zaidi ya 200.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Wilaya ya Mbinga, Erenest Mjirima, alisema kuwa kazi ya jumuiya hiyo ni kuhakikisha wanafunzi wanapatiwa elimu bora pamoja na kutatua changamoto ambazo huwakabili wanafunzi hao hasa wa kike.

Mjirima pia amewataka wanafunzi hao wajitahidi kusoma kwa bidii ili waweze kufanya vema kwenye masomo yao.

Aidha, Naibu Mkurugenzi wa Kampuni ya Ovans Construction Ltd, Agatha Urio, alisema kuwa kampuni hiyo imetoa msaada huo baada ya kupokea maombi kutoka Jumuiya ya Wazazi na kuwa itaendelea kushirikiana na jamii kuona namna ya bora ya kutatua changamoto zilizopo.

# Stanbic yapiga jeki madawati shule Dar

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic imekabidhi madawati 100 yenye thamani ya shilingi milioni 9 kwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, kwa ajili ya Shule ya Sekondari Kijitonyama.

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic, Kevin Wingfield, ndiye aliyekabidhi madawati hayo kwa Gondwe.

Kutokana na msaada huo, changamoto ya madawati shuleni hapo imeisha kabisa kwa mwaka huu.

Mchango huu unakusudia kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya kujifunzia katika shule kote nchini, na kuimarisha msimamo wake kama mshirika aliyejitolea kuboresha elimu Tanzania.

Hafla ya makabidhiano ilifanyika katika eneo la shule wiki iliyopita, na kuhudhuriwa na mwalimu mkuu wa shule, wawakilishi kutoka Manispaa ya Kinondoni, walimu, na wafanyakazi wa benki hiyo.

Wingfield alisema Stanbic imejikita katika kutafuta njia za kuwezesha ndoto na msaada huo utawezesha ndoto za watoto katika Shule ya Sekondari ya Kitonyama. Hatua hiyo inaambatana na kampeni yao inayoendelea ya Stanbic Madawati Initiative ambayo inakusudia kuchangia madawati na miti 1,000 kote nchini ili kuboresha mazingira ya shule, ambayo ni muhimu katika kuchochea ufaulu.

"Mpango wa Stanbic Madawati Initiative unaendana na vipaumbele vya serikali katika kuleta mabadiliko endelevu kwenye sekta ya elimu, msaada huu utawezesha wanafunzi wa hapa kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza. Na zaidi madawati haya yanatengenezwa katika eneo shule ipo hivyo kutoa fursa kwa wanajamii kufaidika na kampeni hii," aliongeza Wingfield.

Kwa upande wake, Gondwe alipongeza juhudi za Benki ya Stanbic katika kusaidia kudhibiti hali ya upungufu wa madawati nchini. "Nina uhusiano mzuri na Benki ya Stanbic na nimefurahishwa sana na juhudi zao za kusaidia jamii. Hii ni benki yenye maono, kwani serikali inavyojenga vyumba vya madarasa lazima hitaji la madawati litaongezeka, mchango huu umekuja kwa wakati muafaka hapa Sekondari ya Kijitonyama," aliongeza.

Kama sehemu ya uwekezaji katika jamii, Stanbic imetoa zaidi ya shilingi bilioni 1 kusaidia sekta ya elimu ya Tanzania; kwa kujenga vyumba vya madarasa, kuchangia madawati, na kukarabati miundombinu ya shule kama vile vyoo ili kuboresha usafi wa mazingira katika shule mbalimbali.

Nipashe
TESA
Jumanne Oktoba 26, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





## Jamii isiyojali elimu ya wasichana inaishi na ulemavu wa kifikra



Ukurasa 12

ZEBAKI INAVYOENDELEA KUTISHIA UHAI MIGODINI

TEKNOLOJIA

NA DINNA MANINGO, TARIME

# Uchakataji kizamani, malighafi ghali upanga unaozichana bidhaa za ngozi

WATU wanajiuliza inakuwaje bidhaa zinazozalishwa nchini zinauzwa ghali wakati zinazotoka nje zinapatikana kwa bei nafuu na kununuliwa kwa wingi kuliko za hapa nyumbani?

Jibu linaweza kuangaliwa kwenye sekta ya ngozi. Takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 zinaeleza kuwa idadi ya Watanzania ni milioni 44. 9.

Wakati takwimu za mifugo zinafahamisha kuwa ni nchi ya tatu kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika, wanaokadiriwa kufikia milioni 30.5, na mapato yake yakichangia asilimia 7.4 ya pato la taifa.

Licha ya kuwapo kwa mifugo mingi bado taifa halijaweza kuwa na bidhaa za ngozi za kutosheleza mahitaji na badala yake, mitumba kuanzia viatu, mikanda, mifuko na nguo vinavyouzwa kwa bei ya chini ndiyo, inayotamba.

Kutokana na kukosekana teknolojia na bei inayovutia wateja wa viatu kikundi cha TAREPA kilichokuwa kinatengeneza viatu vya ngozi kimesambaratika baada ya bidhaa zake kudoda sokoni, anasema Marwa Tongori mmoja wa wana kikundi.

"Nilikuwa msindikaji wa sabuni, mvinyo, baadaye 2009 Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), walitupa mafunzo ya kutengeneza chaki mjini Musoma kwa siku 14, tukatengeneza chaki na kuzipeleka shuleni kupitia waratibu elimu kata, lakini wakazikataa kwa madai ya kuwaumiza macho, wakati huo maduka yalikuwa na punguzo la bei tukakosa wakumuuzia," anasema Tongori.



Bidhaa za ngozi vikiwamo viatu hukosa soko baada ya wateja kukimbilia mitumba. **PICHA: DINNA MANINGO**

"SIDO ilitukusanya tena tuliopata mafunzo ya chaki tukafunzwa kusindika ngozi tukajifunza siku 14, ilitutafutia walimu wakafika Tarime wakatufundisha kutengeneza bidhaa za ngozi," anaongeza.

Anasema biashara ya kutengeneza bidhaa hizo inalipa lakini, imeathiriwa na mtumba huku malighafi za ndani zikiuzwa ghali ikilinganishwa na zinazoagizwa nje na kuongeza: "Tunatoa ngozi kwenye machinjio ya Tarime kilo moja ni Sh.1,200, ya mbuzi ni kati ya Sh. 500-1,500, usindikaji wake ili ukamilike unachukua siku 22. Tunatumia chumvi, chokaa na kuziloweka siku tano, tunaondoa chokaa kwa pumba za mahindi, lakini pumba nazo tunaziondoa kwa kutumia maji ya mapapai ili kuzilainisha na kuzipaka mafuta ya karanga."

"Ngozi ikilainika inapakwa unga wa magome ya mti ili kuiimarisha, magome hayo yanapatikana Mbeya yakiuzwa kilo 50 kwa Shilingi 150,000, halafu hatua za usindikaji zinaanza, ukiwamo umaliziaji wa kuondoa manyoya na nyama zilizosalia kwenye ngozi kwakutumia panga .... " anasema Tongori.

Kinachofuata baada ya hatua hiyo ni kuandaa viatu, kuweka soli, namba, rangi, magongo ya kuweka shepu ili kutengeneza viatu. Pea ya kiatu inauzwa Sh.20,000, gundi ya moto lita tano Sh.3,000,000 inayozalisha viatu pea 50, gundi ya kuunganisha viatu kwenye jointi lita tano Sh.20,000 nyuzi na vifaa vinginevyo," anatoa mchanganuo wa hasara.

**MAUZO YALIVYOKUWA**

Tongori anasema ukosefu wa soko la viatu vya ngozi uliwavunja moyo wanakikundi kutokana na kukaa muda mrefu bila kuuzika, kulikosababisha hasara na kwamba walikuwa wanauza pea nane au 10 kwa mwezi. Viatu vya ngozi vinaogopwa vina bei kubwa hivyo watu kukimbilia mitumba."

Anaongeza kuwa Sh. 5,000 inatosha kununua viatu vya mtumba wakati vya ngozi ni ghali huuzwa Sh. 20,000.

**TEKNOLOJIA DUNI**

Bhoke Marwa mkazi wa mtaa wa Bomani anasema teknolojia za kizamani kutengeneza ngozi hadi kuzalisha viatu hauwavutii wateja, inatoa bidhaa duni na kuchangia wateja kukimbilia viatu vya mitumba.

"Mtumba ina miundo mbalimbali inayomvutia mnunuzi ukitaka cha staili fulani huwezi kukikosa, lakini hivi viatu vya ngozi miundo yake haivutii ni kama vinafanana,ukitaka kiatu cha muundo fulani mpaka ukaweke oda kiwandani, mimi nataka kiatu unaniambia nisubiri wakati kwenye mitumba unakuta kila fasheni," anasema Marwa.

Utaalamu na ujuzi katika kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi nayo imeelezwa kuwa ni sababu inayochangia kushuka kwa soko la viatu vya ngozi kutokana na utaalamu usioendana na wakati na vitendea kazi vya kizamani vilivyopitwa na wakati.

John Chacha mkazi wa mtaa wa Rebu anasema: " Leo tunafanya mambo ya kidijitali lakini bado tunachakata ngozi kwa kuilainisha kwa mapapai, nyama inaposalia kwenye ngozi tunaitoa kwa panga haya ni mambo ya kizamani."

" Matokeo yake kiatu kikitengenezwa baada ya miezi kadhaa kinakuwa kigumu, kinakakamaa kama ngozi iliyokuwa imechunwa ikatupwa juani ikakauka na kukakamaa, nchi haina chuo cha kujifunza uchakataji wa ngozi na utengenezaji wa viatu kwa teknolojia za kisasa ili hawa wenye viwanda vidogo wapate utaalamu wa kisasa ?" anahoji.

**MITUMBA NI TISHIO**

Deo Ching'wa muuza mitumba mtaa wa Serengeti anakiri vimeua soko la viatu vya ngozi vinavyotengenezwa na viwanda vidogo nchini.

"Uzuri wa viatu vya mtumba vina bei zote ya chini ya juu kumwezesha kila mtu kununua kulingana na pesa yake, lakini vya ngozi bei zake si rafiki kwa wenye maisha magumu.

"Ukienda mnadani unapata kiatu hadi cha Sh. 2,000 mwenye kipato cha chini hawezi kushindwa, japo siyo imara lakini ni nafuu atatumia kwamuda akitafuta pesa nyingine, lakini ngozi ni ghali tena kiatu cha hapa Tarime hata kwa Sh. 10,000 hupati. Mtu una watoto watano kipato chako ni cha chini hawezi kununua, unaona hiyo pesa akienda kwenye mitumba anapata viatu pea tano," anasema Ching'wa.

Gharama kubwa za malighafi za kutengeneza ni chanzo cha bei kubwa na kwamba zingepungua wazalishaji wangemudu na wateja wangepatikana, viatu vya ngozi ni imara na vinadumu, anasema.

"Kiatu cha mtumba kimetumika kinaweza kuwa cha ngozi, plastiki au kitambaa lakini vimeshavaliwa kwenye nchi za wenzetu halafu tunaletewa tunauziwa kwa bei ya chini."

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA MARCO MADUHU, KAHAMA

# ZEBAKI INAVYOENDELEA KUTISHIA UHAI MIGODINI

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu wanaendelea kutumia zebaki kuchenjua au kusafisha madini hayo, wakidai ni njia rahisi isiyo na gharama kubwa licha ya Shirika la Afya Duniani (WHO), kusisitiza kuwa ni kemikali hatarishi kwa binadamu na mazingira.

Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), linasimamia utekelezaji wa Mkataba wa Minamata wa kupiga marufuku matumizi ya zebaki duniani ili kulinda watu na mazingira na kutaka mataifa kusimamia kuondolewa kemikali hiyo duniani.

Kuchenjua dhahabu ni kuisafisha na kuitenganisha na taka nyingine na zebaki ndiyo inayotumiwa kwa vile dhahabu inanasa kwenye kemikali hiyo kama sumaki inavyovuta chuma.

Wachimbaji wadogo nchini wanakadiriwa kutumia takribani takriban tani 24.4 ya zebaki kwa mwaka na katika mchakato huo hakuna tahadhari.

Utafiti unaofanywa na Nipashe kwenye migodi ya Nyarugusu mkoani Geita na Mwime Shinyanga, unathibitisha kuwa wachimbaji hawajali vifaa kinga.

Wakati mwingine huchenjulia karibu na mto, maziwa na kwenye mikondo ya maji na kuchafua mazingira kwavile zebaki inazama majini.

Katika mgodi wa Mwime uliopo Manispaa ya Kahama, wachimbaji hujaza mchanga wa dhahabu kwenye makarai yenye maji na zebaki na kuanza kuchenjua lakini mikononi na miguuni hawana kinga na kuruhusu kemikali hiyo hupenya mwilini.

Aidha, dhahabu hiyo ikijishika kwenye zebaki huchoma ili kuisafisha lakini mvuke hupenya kwenye mfumo wa hewa na kuzidi kuchafua mazingira na kuumiza mapafu.

Mgodini Mwime mchimbaji Fred Fikiri, anasimulia jinsi zebaki ilivyoathiri afya za wachimbaji waliokuwa wanachoma dhahabu yenye zebaki kwenye mkaa ili kuisafisha.

Anasema walifanya kazi hiyo muda mrefu bila kuvaa barakoa, lakini hawakufahamu kuwa ina madhara na kuongeza:

"Wakati wa kuchoma dhahabu kwenye moto, mvuke wa zebaki hutoka na sisi tulikuwa tukiuvuta tukiona kama kitu cha kawaida, bila ya kujua unadhuru mapafu na ngozi zetu," anasema Fikiri.

"Kutokana na kufanya kazi kwa muda mrefu, mwenzetu mmoja alianza kukohoa tukajua kikohozi cha kawaida lakini akazidiwa vipimo hospitalini vikaonyesha kuna matatizo ya athari za zebaki.

"Akaanza matibabu lakini akapoteza maisha, ndipo na mimi nikaogopa nimeanza kuvaa barakoa wakati wa kuchoma dhahabu ili nisivute moshi na mvuke wa zebaki wenye sumu," anaeleza Fikiri.

Deogratius Laurent anaendelea kuchenjua dhahabu kwa zebaki hapo Mwime, anasema mara nyingi hawatumii vifaa kinga lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa elimu ya madhara ya zebaki na kwamba hawayaoni zaidi ya kusikia.

Anahisi wachimbaji wengi wameshaathirika hata yeye akisema anachoona ni kutetemeka mikono na kukosa nguvu.

Anaungwa mkono na Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo wa Mkoa wa Madini Kahama Joseph Andrew, anayesema wachimbaji wengi hawana elimu ya madhara ya zebaki na kila siku wanaibuka wapya migodini, lakini hata wakielimishwa wanakataa vifaa kinga na hata wakipewa wanavipuuza kwasababu madhara yake hayaonekani kwa haraka bali baada ya miaka mingi.



Deogratius Laurent, akichenjua dhahabu kwa kutumia zebaki, mbele ya wajumbe wa Kamati ya Bunge, Viwanda, Biashara na Mazingira, waliozuru mgodi mdogo wa Mwime uliopo Kahama, kuchunguza athari za kemikali hiyo. **PICHA : MARCO MADUHU**

**ZEBAKI KUONDOLEWA**

Mkurugenzi Msaidizi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Onesphory Kamkuru, anasema serikali imeanza mpango wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo, kwa asilimia 30 kiwango kitakachoifikiwa ifikapo 2025.

Anasema mpango huo umelenga kutumia teknolojia rafiki ambayo haiwezi kuleta madhara ya kiafya kwa binadamu, na kuachana kabisa na zebaki.

"Mpango kazi wa taifa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu 2020-2025, umeandaliwa na kukidhi matakwa ya mkataba wa Minamata, mji wa Japan, ambao madhara ya zebaki yalianza kuonekana," anasema Kamkuru.

Anasema mkataba huo ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2016 kwa kuandaa mpango kazi unaolenga kuwa ifikapo mwaka 2032 hakutakuwapo zebaki kwenye migodi nchini. Pia, anasema asilimia 25 hadi 35 ya wachimbaji wadogo wa dhahabu wameathiriwa na kemikali hiyo.

Anasema kutokana na kemikali hiyo kuwa na madhara kwa afya ya binadamu, serikali imeanza kufanya utafiti wa kupata teknolojia mbadala itakayoiondoa zebaki migodini.

**ATHARI ZA ZEBAKI**

Ofisa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Joseph Bilago, anazitaja kuwa ni pamoja na kutetemeka, kulegea misuli, kusahau, kukosa nguvu na maumivu ya kichwa mara kwa mara.

"Athari zinarithiwa zinaweza kuathiri vizazi na vizazi, kusababisha kuzaa watoto wenye ulemavu, yenye uwezo mdogo wa kufikiri na hata kupata mtindio wa ubongo ukubwani."

Hivi karibuni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, akiwa kwenye mgodi wa Mwime, anaeleza kuwa wagonjwa wengi wa saratani walioko kwenye Taasisi ya Saratani ya Ocean Road Dar es Salaam, watoka mikoa ya kanda ya ziwa, na hiyo inatokana na matumizi zebaki kwenye machimbo ya dhahabu.

Waziri anawataka wachenjuaji na wachomaji wa dhahabu, wachukue tahadhari ya kemikali hiyo, kwa kuvaa vifaa kinga, ikiwamo barakoa, glovu na buti ili kujilinda na zebaki, wakati serikali inaendelea kutafuta njia mbadala.

Anaawaagiza wataalamu wa mazingira kutembelea ya migodi midogo ya dhahabu kutoa elimu kwa wachimbaji ili kuchukua tahadhari ya zebaki na kuepusha madhara zaidi.

# Uchakataji kizamani, malighafi ghali upanga unaozichana bidhaa za ngozi

**INATOKA UK.11**

"Kuna viatu vya ngozi vya mtumba vinauzwa mpaka Sh. 100,000 au zaidi, watu wananunua lakini ni wachache, wanaovielewa na wenye kipato kikubwa, wanaotengeneza viatu vya ngozi wajitahidi viwe imara na mwonekano mzuri, muundo unaovutia na unaokwenda na wakati," anashauri Ching'wa.

Ramadhani Khalfan ni fundi bidhaa za ngozi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) tawi la Mwanza, anasema taasisi hiyo ina chuo kinachotoa mafunzo ya kuchakata ngozi na kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi.

" DIT tunachakata ngozi zikiwamo za wajasiriamali, kama wanaweza kukusanya ngozi wanaruhusiwa kuzileta wakati wowote, gharama ya kuchakata ni ya ng'ombe Sh. 25,000, mbuzi 5,000 na tunafundisha kuanzia kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi," anasema.

Kuna kozi fupi, zipo za miezi miwili na za kutengeneza viatu, zote hutolewa kwa miezi miwili na kila kozi hugharimu Sh. 300,000, anasema.

Anaongeza kuwa zipo kozi za muda mrefu ambazo ni ya kuchakata ngozi na kutengeneza bidhaa inyoanza mwaka huu nakwamba DIT Mwanza ni chuo pekee nchini kinachotoa mafunzo ya ngozi kwa ngazi ya diploma.

Godfrey Chasama ni mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) anasema kuwa Tanzania inazalisha ngozi ghafi na kwamba bei ya ngozi ghafi ni 4,500 inayotoa jozi tano za viatu, bei ya jozi ni Sh.14,000 uwezo wa kuzalisha ni jozi 240 kwa mwezi.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Wakazi Dar es Salaam wanavyoamka kuchunguzwa, kuelimishwa saratani

KUHAMASIKA na kujali afya ni kila kitu. Ndivyo unavyoweza kusema kufuatia mwitikio mkubwa wa wakazi wa Dar es Salaam, wanaojitokeza kuchunguza na kutibu saratani mapema.

Wanafanya hivyo, kupitia Kampeni ya Afya Kwanza yenye kauli mbiu ya Shtukia Fasta, inayolenga kuwachunguza watu saratani, kuigundua mapema na kuitibu ili kuepusha madhara. Idadi kubwa ya wananchi wamejitokeza kupima afya zao.

Taasisi mbalimbali za kijamii pamoja na serikali zinashirikiana kupima wananchi lengo likiwa kupunguza tatizo la saratani nchini, anasema Dk. Irene Ketegwe.

Akizungumza katika ufunguzi wa kambi ya kwanza ya siku mbili ya upimaji saratani bure Mbagala, Dk. Irene kutoka Taasisi ya Tanzania Comprehensive Cancer Project ( TCCP), ambayo pia ni mdau kufanikisha upimaji anasema, kazi hiyo inatazamiwa kupunguza gharama kubwa ya matibabu inayotokana na kuchelewa kugunduliwa mapema.

Hatua hiyo inafanyika kutekeleza utaribu wa kimataifa wa kuchunguza na kuongeza ufahamu wa saratani ya matiti duniani, inayofanyika Oktoba kila mwaka.

Dokta Irene, anasema taasisi zinazofanikisha uchunguzi huo ni pamoja na Inspire Consultants, Associazione Ruvuma Onlus, Shujaa Cancer Foundation, Genesis Cancer and Palliative Care Foundation, Tanzania Comprehensive Cancer Project na Ocean Road Cancer Institute.

Anasema upimaji huo unafanyika bila malipo, kwa wakazi wa maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika ufunguzi mtaalamu huyo, anasisitiza kuwa lengo ni kupunguza gharama kubwa ya matibabu ambayo ingetokana na maradhi kuchelewa kugundulika.

Aidha, jitihada hizo zinapunguza idadi ya vifo kwa sababu watu watawahi kutibiwa.




Huduma ya upimaji wa saratani ya matiti, shingo ya uzazi na tezi dume ukiendelea katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### SARATANI YA KIZAZI

Dokta Irene akiizungumzia anaeleza kuwa matibabu ya saratani hiyo hutolewa kulingana na hatua za ugonjwa na hali ya mgonjwa na kwamba upasuaji katika hatua za mwanzo hufanyika, mionzi, dawa za saratani au mionzi na dawa kwa pamoja hutolewa.

Anasema gharama zake huwa mara dufu endapo mgonjwa anachelewa kugundulika.

Anataja dalili kuwa ni pamoja na kutokwa na damu baada ya kujamiiana, kutoka uchafu, au majimaji yenye harufu mbaya, ama usaha sehemu za siri.

Nyingine ni kuona damu isiyo ya hedhi, au kutokwa na damu baada ya kukoma hedhi, maumivu ya kiuno na tumbo chini ya kitovu na kuwataka wawahi hospitali kwani hizo ni dalili za saratani ya mlango wa kizazi.

Mkurugenzi wa Kinga wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Crispin Kahesa, anasema: "Kansa ya mlango wa kizazi inaoongoza kwa vifo vingi vya wanawake nchini, hivyo utaratibu wa kupima utasaidia kuvipunguza kwani ikigundulika mapema inatibika."

Aidha, anawaonya wanaojitokeza kupima kuchukua tahadhari za kujikinga na kuacha kujamiana na wanaume wengi kwani kirusi cha ugonjwa huo kinasambaa kwa njia ya kujamiana na mtu mwenye kirusi hicho.

Wanaume wanaojamiina na wanawake wenye virusi hivyo wanaweza kuvisambaza kwa kinamama wengine.

Akizungumzia mwitikio wa Kampeni ya Afya Kwanza, Mratibu wa Upimaji Happy Rwechungura, anasema wananchi wengi wameamka na kuona umuhimu wa wanaojitokeza kupima afya zao.

"Tunaowakuta na matatizo tunawapa barua ya kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road ili kuendelea kupata uchunguzi na tiba endelevu."

Baadhi ya wakazi wa Mbagala, Tabata, Kigamboni waliojitokeza katika kambi ya kupimaji viashiria vya saratani ya matiti, mlango wa kizazi na tezi dume, waliogundulika na viashiria vya kansa walipatiwa rufani ya kwenda kupima zaidi Ocean Roada.

Wakazi wa maeneo mengine ya Dar es Salaam, wataendelea kupimwa bila malipo katika kambi mbalimbali hadi Oktoba 29.

Vituo hivyo ni Kimara Stop Over kilichoanza jana, Tanganyika Packers kitakachoanza kuhudumia Alhamisi na Ijumaa wiki hii kwa wananchi kuchunguzwa saratani za tezi dume, matiti na mlango wa kizazi.

Mmoja wa wanufaika wa huduma ya upimaji wa saratani ya matiti na mlango wa Fatuma Mikidadi anasema ni nzuri na kuomba muda uongezwe ili kufikia wengi.

"Huduma ni nzuri lakini siku mbili hazitoshi kwa sababu watu ni wengi na wengine bado hawana taarifa hivyo wakisikia watakuwa wengi," anasema .

Takwimu kutoka Mbagala Zakhiem zoezi hili lilipoanzia, zinaeleza kuwa watu zaidi ya 300 walikuwa wamechunguzwa na kwamba kutokana na wingi wa watu wanakusudia kuwafikia wananchi 3,000 kwa muda wa siku 10.

"Tulianza shughuli saa moja lakini hadi kufikia saa 4:30 asubuhi tumeshaandikisha watu zaidi ya 300 kwa siku hizi mbili tunaweza kuwafikia takribani watu 600," anasema.

Mratibu Mwandamizi wa Mradi, Nseya Kipilyango kutoka Taasisi ya Inspire Consultants.

Anaeleza kuwa idadi kubwa ya waliojitokeza ni wanawake, hata hivyo ameshangazwa na idadi kubwa zaidi ya wanaume hasa ukichukulia kuwa kutokana na dhana potofu kuhusu upimaji mwanzoni wanaume wengi waliogopa kujitokeza. Anasema uelimishaji unaoendelea katika vyombo vya habari umesaidia kuongeza idadi ya wanaume kushiriki kupima tezi dume uchunguzi unaofanyika kwa njia ya damu.

"Tunashukuru serikali kwa kutupatia maeneo ya kutoa huduma hizi, changamoto kubwa tuliyokutana nayo ni watu wengi wanajitokeza, na kuonyesha kuwa kuna uhitaji mkubwa lakini uwezo wetu ni mdogo, tunaomba watu na taasisi mbalimbali kujitokeza kuchangia ili tuweze kufikia watu wengi zaidi."

"Tuna uhitaji 'PSA Kits' kwa ajili ya kuchunguza tezi dumu kwa wanaume wanaopimwa damu, mahema ya wagonjwa kusubiri, tunahitaji wataalamu wa Ultrasound, madaktari na wauguzi kupunguza gharama za uendeshaji, wa kujitolea ili mapambano yawe endelevu kuisaidia serikali kupambana na saratani."



ELIMU
NA MASHAKA MGETA, HANDENI

RC MALIMA:

# Jamii isiyojali elimu ya wasichana inaishi na ulemavu wa kifikra

WAKATI harakati za kutetea haki za mtoto wa kike zikiendelea kwa kasi duniani kote, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, anaziambia jamii zenye wasichana wasiokwenda shule kuwa zinaishi na ulemavu wa kifikra.

Anayasema hayo, alipoitembelea Sekondari ya Wasichana Handeni, mkoani Tanga na kusema jamii zilizofanikiwa kuwekeza kuwaelimisha wasichana, zimepiga hatua kimaendeleo na kifikra, wakati zinazokandamiza haki ya kupata elimu zinazidi kudumaa.

Mkuu wa Mkoa Malima anasema, pamoja na hali hiyo, wasichana wanaopata nafasi za kuendelezwa kielimu katika hatua zozote, wanapaswa kutambua namna familia na jamii zao zinavyowategemea, hivyo watumie fursa hizo kujenga misingi imara ya kuwa na maisha bora baadaye.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga Adam Malima. **PICHA MTANDAO.**

**ACHENI KUDANGANYIKA**

Anakumbusha kuwa baadhi ya wasichana wanafunzi wamekuwa na kasumba ya kujihusisha na mambo maovu yaliyo kinyume na matarajio ya wazazi, walezi au jamii wanazotoka na kushindwa kuendelea na masomo.

Akitoa mfano, anasema baadhi ya wanafunzi hao hudanganywa na vijana wakiwamo wanaoendesha bodaboda, kiasi cha kujikuta kwenye uhusiano wa kimapenzi na baadaye kukatisha masomo kutokana na ujauzito.

"Vishawishi wanavyotumia kuwarubuni wasichana shuleni ni pamoja na kuwapa chips mayai au kuku. Yaani msichana msomi unafikia hatua ya kulaghaika na kujiharibia masomo kisa Shilingi 2,000...," anawaasa Mkuu wa Mkoa na kuongeza kuwa wanaopata fursa ya kuendelezwa kielimu, wanapaswa kuwa mfano bora kwa wengine.

**MATARAJIO YA JAMII**

Aidha, Malima anasema wanafunzi wa kike wanashindwa kuendelea na masomo hasa kutokana na ujauzito, wanakuwa sehemu ya vyanzo vya kusababisha ndoa nyingi kuvurugika kwa sababu ya lawama zinazoelekezwa kwa mmoja wa wazazi ama walezi kwao.

"Mnapopata ujauzito na kushindwa kuendelea na masomo mtambue kwamba hata ndoa za wazazi ama walezi wenu zinayumba huko nyumbani, baba anaweza kumshutumu mama kuwa ni chanzo na wakati mwingine mama anaweza kumnyooshea kidole baba, kwa sababu tu amempenda sana binti yake kiasi cha kumdekeza," anawaeleza na kuwaasa, subira yavuta heri.

**RAIS SAMIA KIELELEZO**

Malima anatoa mfano wa viongozi kadhaa waliokuwa wasichana, wakautumia vema ujana wao kujiendeleza na hivi sasa wana nafasi kubwa za uongozi, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mnapomwona Mama yetu, Mheshimiwa Rais, amekwenda shule na kufuzu hadi vyuo vikuu, anakuwa mfano bora kwenu, kuona manufaa ya kusoma kwa bidii pasipo kudanganyika. Matarajio yake ni kuwaona mnafaulu vema," anasema na kuongeza kuwa wasichana wana thamani kubwa katika familia na jamii, hivyo wanastahili kutambua thamani zao na kujiheshimu.

Malima anatoa onyo kwa wanaowalaghai wanafunzi wasichana wa shule za msingi na sekondari akisema katika uongozi wake mkoani Tanga, atahakikisha wanachukuliwa hatua kali za kinidhamu, kimaadili na kisheria, ili kuwa fundisho kwa sehemu nyingine za nchi.

"Ninawaonya wanaojihusisha na ulaghai dhidi ya wasichana waliopo mashuleni, wakikamatwa, nitakachowafanya kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kitakuwa ni fundisho kwa wengine ndani na nje ya Tanga," anasema.

**DC APONGEZA**

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, akielezea kufurahishwa na juhudi hizo anasema shule hiyo ni miongoni mwa shule tatu za sekondari za kidato cha tano na sita zilizoanzishwa mwaka jana na kuanza kuchukua wanafunzi ulipoanza muhula huu wa masomo.

> "Vishawishi wanavyotumia kuwarubuni wasichana shuleni ni pamoja na kuwapa chips mayai au kuku. Yaani msichana msomi unafikia hatua ya kulaghaika na kujiharibia masomo kisa Shilingi 2,000…," anawaasa Mkuu wa Mkoa na kuongeza kuwa wanaopata fursa ya kuendelezwa kielimu, wanapaswa kuwa mfano bora kwa wengine.

Mbali na Handeni, nyingine ni Sekondari za Ndolwa na Misima na kuongeza kuwa moja ya vipaumbele vyake ni kuhakikisha changamoto zinazowakabili wanafunzi wa kike wilayani Handeni zinatatuliwa na kuifanya wilaya hiyo kuwa mahali salama kwa msichana kuelimika.

Ofisa Tarafa ya Sindeni iliko sekondari hiyo, Sijaona Bugufi, anasema kabla ya kusajiliwa, majengo ya shule hiyo yalikuwa ofisi za shirika lisilokuwa la kiserikali la World Vision na baadaye kugeuzwa kuwa chuo cha ufundi.

Anasema mwaka 2019, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya, Toba Nguvila na watendaji akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, William Makufwe, walihimiza kasi ya kukifanya chuo hicho kuwa sekondari ya wasichana, pamoja na shule za Misima na Ndolwa.

"Toba alipofika hapa Handeni alitangaza ujenzi wa shule za sekondari za kidato cha tano na sita kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vyake, na kwa kushirikiana na watendaji wa halmashauri na wilaya, azma hiyo ikafanikisha kusajiliwa kwa shule hizo tatu," anasema.

**WANAFUNZI WANENA**

Wanafunzi 69 wa Sekondari ya Wasichana Handeni, wanautaja ujio wa Mkuu wa Mkoa Malima kama kichocheo cha kujikita katika masomo na kukabiliana na vikwazo.

Wanasoma michepuo ya Historia, Kiswahili na Lugha (HKL) na Historia, Jiografia na Lugha (HGL) ambayo, Mkuu wa Mkoa Malima anapendekeza iongezewe michepuo ya sayansi.

Wakizungumza kwa niaba ya wenzao, wanafunzi wa Sekondari ya Handeni, Asha Salehe na Martha Reuben wanaelezea matatizo kadhaa yanayowakabili, na kuomba kupewa kipaumbele kuyatatua.

Wanataja upungufu wa vitabu unaowafanya washindwe kufuatilia kwa ufanisi mafunzo wanayoyapata kutoka kwa walimu wao na kwamba wana idadi ndogo ya vitabu isiyotosheleza mahitaji na kuomba msaada, lakini pia wakigusia mabweni kukosa uzio na kuwaweka katika mazingira magumu kama kuzingirwa na wanyama.

Mkuu wa Mkoa Malima anasema, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa vitabu, atashirikiana na Mbunge wa Handeni vijijini, John Salu kununua kopyuta, nyenzo za mtandao wa mawasiliano ya kielektoniki na mashile za kudurufu, ili vitabu vinavyopatikana mtandaoni vichapishwe na na kusambazwa kwa wanafunzi hao.

Kuhusu ujenzi wa uzio wa shule hiyo, Malima anasema baada ya Mbunge Salu kukubali kuwa mlezi wa shule hiyo, atashirikiana naye kuweka mipango itakayofanikisha ujenzi huo.

**Mwandishi ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga. Mawasilino: 0754691540.**

## PAC yazungumzia majibu TANROADS

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imesema Wakala wa Barabara (Tanroads) umewawilisha majibu kuhusu hoja mbalimbali za ukaguzi ikiwamo maelezo ya kina ya kimaandishi kuhusu matumizi ya Sh. bilioni 616.3 bila idhini ya Bunge.

Wakala huo uliagizwa na kamati hiyo kuwasilisha maelezo hayo wiki iliyopita baada ya kutowasilishwa kwa wakati nyaraka zilizopaswa kufanyiwa kazi na kamati hiyo kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza jana na Nipashe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alikiri kuwa amejulishwa na Katibu wa Kamati hiyo kuwa Tanroads wamewasilisha ripoti waliyoagizwa..

"Hivyo Tanroads wametekeleza matakwa ya kamati kama walivyotakiwa hivyo tunapanga muda, sisi kama kamati kukaa kuangalia majibu yao kama yanakidhi vigezo," alisema.

Alisema matakwa ya kamati yametimizwa lakini kuhusu majibu ya hoja walizojibu Tanroads ni hadi hapo kikao cha kamati kitakapokaa na kutoa majibu kama imeridhika au haijaridhika.

Oktoba 18, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka alisema Wakala huo katika hoja za ukaguzi zinazoishia Juni 30, mwaka 2020 umefanya matumizi mabaya ya Sh.Bilioni 616.3 kinyume cha taratibu bila kuidhinishwa na Bunge na kutaka majibu ya hoja zilizoibuliwa kuwasilishwa Oktoba 20, mwaka 2021.

Alisema haiwezekani kutumia fedha ya umma zaidi ya ile iliyopitishwa kwenye bajeti kama hawajapata kibali cha Bunge.

"Tumewaagiza watuletee kwa maandishi aliyeidhinisha kutumika kwa kiasi hicho cha fedha na kufanya matumizi hayo bila kibali cha bunge," alisema.

Kuhusu kutofanyika kikao, Kaboyoka alisema "nyaraka huwasilishwa na CAG, lakini tumezipata tukiwa kwenye kikao, tulijua kwamba hatutaweza kutendea haki kazi hii kutokana na kwamba Sheria ya Bunge ambayo inatufanya tufanye vikao inataka kwamba nyaraka zote, ripoti ya CAG kuhusu miradi mbalimbali ambayo tunasimamia iwasili kwa kamati siku tatu kabla ya kikao husika."

"Hii inawapa wajumbe nafasi ya kusoma nyaraka kuzielewa, kutafuta ufafanuzi zaidi ili tutendee haki bunge lililotupa wadhifa huu wa kusimamia fedha za umma kwa hiyo tumewarudisha,"alisema.

Alisema Ofisi Masuuli ambaye ni Katibu Mkuu wa Ujenzi alizuia kuwasilishwa kwa nyaraka hizo kwa kamati akidai kuwa zina marekebisho.

"Kutokana na kutaka ile document ibebe maudhui aliyotaka Ofisi ya CAG ikaona basi tungoje maana ofisa masuuli ndio kasema hili na lile, kusema kweli aliyechelewesha kazi hii ni Katibu Mkuu wa Ujenzi maana CAG asingemkatalia kuwasilisha hayo marekebisho na ndio mwajibikaji mkuu katika kamati hii na ndio anayejibu hoja za bunge," alisema.

# Watumishi wafundwa matumizi ya mikopo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATUMISHI wa serikali wametakiwa kutumia vizuri mikopo wanayochukua kwenye vyama vya akiba na mikopo vilivyoko kwenye maeneo yao ya kazi ili kujikwamua kiuchumi.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Allan Kijazi, alitoa wito huo jana alipokuwa akifungua mkutano wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Wizara hiyo (MNRT Saccos Ltd) jijini hapa.

"Kwenye mikutano kama hii utasikia mtu analalamika viongozi hawa ni wabaya au saccos hii haitufai kumbe amekopa na fedha alizopata alizitumia kwa anasa bila kuwekeza au kuanzisha mradi," alisema.

Kadhalika, aliwahamasisha kutumia fursa hiyo ya mikopo kwa kufanya kazi kwa bidii na kujituma ndiyo chachu ya kujiletea maendeleo endelevu binafsi na Taifa kwa ujumla.

Katibu Mkuu huyo alisema wizara ipo kusimamia kuimarisha Sekta ya Ushirika ili watumishi wengi wajikwamue kiuchumi na kuwataka viongozi wazitunze vyema fedha za wanachama. Alitoa wito kwa watumishi wa Wizara na Taasisi za Wizara ambao hawajawa wanachama kujiunga na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ili kuwawawezesha kujitunzia akiba ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa MNRT Saccos Ltd, Dk. Christowaja Ntandu, alisema chama hicho kilianzishwa mwaka 2014 na kilianza na mtaji wa Sh. milioni mbili tu na hadi sasa mikopo ya Sh. milioni 253.7 imetolewa kwa wanachama 46.



Mkurungenzi wa Taasisi ya Mkapa Foundation, Dk. Ellen Mkondya Senkoro, akizungumza na wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kwenye semina iliyofanyika jijini Dodoma jana, iliyoandaliwa na taasisi hiyo.
**PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Shirika lilivyowawezesha vijana 120,000

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha mwaka 2020, Shirika lisilo la kiserikali la Restless Development, limewajengea uwezo wa kujiajiri, kuibua fursa mbalimbali na kuzifanyia kazi vijana zaidi ya 120,000 nchini.

Meneja ufuatiliaji maendeleo ya miradi wa Shirika hilo, Nassor Kikumbih, alibainisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI) jijini hapa.

Alisema katika moja ya miradi inayotekelezwa na shirika hilo ni kusaidia vijana kujiajiri na kuibua fursa zilizopo na kuzifanyia kazi.

Alieleza kuwa katika mradi huo wamekuwa wakitoa mafunzo kwa vijana namna ya kuibua miradi yao ya biashara na kuwasaidia kuiboresha na kuipeleka serikalini kwa ajili ya kupata mikopo.

"Wanaibua miradi, lakini na sisi tunakuwapo kurekebisha kile walichokiibua ili wanapoipeleka katika maeneo mbalimbali wanapatiwa mikopo ikiwamo ile ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri," alisema.

Pia alisema mafunzo mengine wanayowapatia vijana ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kuweza kujenga hoja kuhusu haki zao kwa watunga sera.

"Tunawapatia uwezo wa kujenga hoja kwa watunga sera, lakini wakiwa na data ya kile wanachokidai na hii inawasaidia viongozi wakiwamo wakurugenzi kuwasikiliza kutokana na data walizonazo."

"Hatutaki kujenga vijana ambao wanalalamika katika social media tuu tunataka kuwa na vijana wenye hoja wanapotoa kitu wanakuwa na data kama ni kukosa mikopo wanaainisha kabisa ni watu gani wamekosa na wakurungezi wanafanyia kazi," alisema.

Vilevile, alisema mafunzo mengine wanayoyatoa ni kuwajenga vijana kuwa viongozi wa leo na kesho.

"Asilimia 60 ya watu nchini ni vijana hivyo lazima tuwatengeneze vijana kuwa viongozi wa sasa kuanzia ngazi ya chini kabisa," alisema.

Alisema kijana anatakiwa kuwa kiongozi kuanzia katika eneo lake analoishi kwa kushiriki shughuli mbalimbali ikiwamo zile za majanga.

"Kama leo yametokea mafuriko hata yakasomba nyumba katika eneo lake kijana anatakiwa kuwa mstari wa mbele kwenda kushiriki kutoa msaada hata ikitokea uchaguzi jamii lazima itakuwa na imani na kijana anayejitolea na kumchagua," alisema.

Kadhalika, alisema mafunzo mengine ni afya ya uzazi na makuzi ambapo wamekuwa wakitoa elimu kwa makundi ya wavulana na wasichana ili kupunguza tatizo la mimba katika umri mdogo.

"Mkimpa elimu ya uzazi na makuzi kijana wa kiume pekee yake unakuwa hujafanya jambo bali wanatakiwa kupata wote ili hata mwenziwe anapokuwa katika wakati hatari wa kupata mimba akimwambia anaelewa kwasababu elimu anayo," alisema.

Alisema kitendo cha mvulana kumlazimisha msichana kufanya naye ngono akiwa katika kipindi cha hatari ya kupata mimba huo ni ukatili wa kijinsia hivyo elimu ndiyo inatakayo saidia kuondokana na ukatili huo.





# 118 mbaroni kuingia nchini kinyemela kwa miezi mitatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHAMIAJI haramu 118 kutoka katika mataifa mbalimbali wamekamatwa na maofisa wa Uhamiaji mkoani Mbeya katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai mpaka Septemba mwaka huu.

Wengi wao wanadaiwa kuingia nchini kupitia njia za panya.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Kigongo Shikille, alisema wahamiaji hao walikamatwa kufuatia uperesheni maalum iliyofanyika katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema operesheni hiyo ilifanyika maeneo ya mpakani, kwenye vituo vya mabasi pamoja na kwenye maeneo ya migodi na sehemu zingine za ajira ambako wengine walikutwa wakiwa wanafanya kazi bila kuwa na vibali.

Alisema kati ya wahamiaji hao haramu waliokamatwa, 85 walikuwa ni raia wa Malawi na wengine 33 walikuwa ni kutoka katika mataifa mengine.

Alisema waliamua kufanya operesheni hiyo ambayo ilikuwa ya kushtukiza katika maeneo mengi kutokana na kukithiri kwa raia wa kigeni kuingia nchini kupitia vipenyo visivyokuwa rasmi maarufu kwa jina la njia za panya.

"Tulilazimika kufanya operesheni maalum baada ya kubaini ongezeko la wahamiaji haramu kuingia nchini, makundi haya wakati mwingine yanakuwa hatari kwa sababu hatujui wanaingia na vitu gani ama wana magonjwa gani," alisema Shikille.

Alisema baadhi ya raia hao wa kigeni wamekuwa wakiingia nchini na kuanza kufanya shughuli zao za uzalishaji mali na wengine kuajiriwa katika maeneo mbalimbali ikiwamo mashambani na kwenye migodi pamoja na wafanyakazi wa majumbani.

Shikille alisema mbali na kufanya zoezi hilo pia wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye magari makubwa ya mizigo na abiria ambayo yamebainika kuwa vinara wa biashara haramu ya kusafirisha binadamu hususani wahamiaji haramu.

"Kwa sasa tutakuwa wakali sana kwa sababu kuna katabia kameibuka kwa raia wa kigeni kuingia nchini kinyume cha utaratibu na wengine wanasaidiwa na Watanzania wenzetu, Watanzania tujuwe kwamba kufanya hivyo ni kujihatarisha maisha yetu wenyewe," alisema Shekille.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wananchi mkoani Mbeya walisema katika Mkoa huo kumekuwa na tatizo kubwa la raia wa kigeni kuingia na kufanya kazi mbalimbali za ndani pamoja na wahudumu wa bar.

Joseph Mwangupili alisema kwa sasa yapo magonjwa mengi ambayo ni hatari na yanaweza kusambaa kutoka taifa moja kwenda lingine kupitia wahamiaji ambao hawadhibitiwi.

Alisema kwa sasa dunia inakabiliwa na tatizo la ugonjwa wa corona ambao ni hatari na kwamba kuna uwezekano wahamiaji hao wakawa chanzo cha kusambaa kwa ugonjwa huo nchini.

Naye Frozia Sabuni aliviomba vyombo vya ulinzi na usalama viongeze usimamizi wa mipaka pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kuwahifadhi wahamiaji hao akidai kuwa baadhi ya wananchi wamekuwa wakiwahifadhi na wengine kuwaajiri.



Baadhi ya wanawake wa Mwambene katika Kata ya Mwakibete jijini Mbeya wakiwa wamejitwisha ndoo za maji juzi, ambayo wanachota kwenye chanzo cha Mto Nzovwe kutokana na eneo lao kutokuwa na maji ya bomba kwa zaidi ya siku tatu sasa. **PICHA; NEBART MSOKWA**

## Bil. 1.3/- kujenga vyumba madarasa Wilaya ya Chunya

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.3 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 65 vya madarasa.

Madarasa hayo yatajengwa kwenye shule za msingi shikizi na shule za sekondari zilizoko wilayani humo.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na serikali pamoja na wadau mbalimbali wilayani humo.

Alisema baada ya fedha hizo zimeshaingia na kuanza utekelezaji wa miradi ya sekta hiyo elimu kwa kuanza ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule hizo.

"Fedha hizo zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan na kwa mtazamo wangu zitakuwa kichocheo cha kupunguza tatizo la mrundikano wa wanafunzi shuleni, pia itasaidia kuinua kiwango cha elimu katika Wilaya yetu," alisema Kasaka.

Alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na madawati na kupitia fedha hizo kwa mwaka ujao wanafunzi wote watasoma katika mazingira salama na kuongeza ufanisi katika elimu.

Alisema wananchi pia wanashirikishwa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kuchangia nguvu zao kufyatua tofali na kubeba mchanga na mawe.

Vilevile alisema miradi hiyo inatekelezwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura maarufu kwa jina la Force Account ambao unaharakisha utekelezaji wa miradi.

Hivi karibuni, serikali ilitoa fedha kwenye mikoa yote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hasa miradi ya afya na elimu.

# Ufumbuzi uzalishaji mdogo wa mpunga mbioni

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

TATIZO la uzalishaji mdogo wa mpunga kwa wakulima wa Wilaya ya Kyela, linaelekea kupata ufumbuzi wa kudumu baada ya utafiti wa mbegu chotara zenye kuhimili, kukinzana na magonjwa na kutoa mavuno mengi kukaribia kukamilika.Utafiti huo unafanywa wa mbegu unafanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Dakawa mkoani Morogoro kwa kushirikiana na wadau wa utafiti wa mbegu za mpunga kutoka nchini Kenya.

Utafiti huo unafanyika katika shamba la utafiti wa mpunga lililoko katika Kijiji cha Ngana kilichopo katika Mji wa Kasumulu wilayani Kyela ambako maofisa hao wamepiga kambi.

Mwakilishi wa Tari kutoka kituo cha Dakawa, Barnabas Sitta alisema mbegu wanazozifanyia utafiti zitasaidia kuongeza uzalishaji wa mpunga katika Wilaya ya Kyela pamoja na maeneo mengine ambayo watasambaza mbegu hizo.

Alisema mbegu hizo ni bora kwa sababu zinavumilia ukame pamoja na kuwa na uwezo mkubwa wa kukinzana na magonjwa na hivyo zitawasaidia wananchi kupunguza gharama za uzalishaji wa zao hilo hasa katika maeneo yenye ukame.

Sitta ambaye ni mtafiti wa mpunga, alisema maeneo mengi ya Wilaya ya Kyela wakulima wamekuwa wakitegemea mvua na hivyo mvua ikiwa kidogo ama ikichelewa kuanza mazao yao yamekuwa yakinyauka na hivyo mbegu wanazozifanyia utafiti zitakuwa suluhisho. Aliwataka wakulima wa mpunga kuzingatia mbinu za kilimo bora cha zao hilo ili waongeze tija kwenye uzalishaji pamoja na kuinua uchumi wao na wa taifa kwa ujumla.

"Wakulima wamekuwa wakizalisha kwa kiwango ambacho ni kidogo ukilinganisha na maeneo wanayolima, sasa kwa mbegu hizi tukimaliza utafiti ambao nina imani unakamilika hivi karibuni wataongeza uzalishaji mara dufu," alisema Sitta.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Shirika la Kilimo la African Agricultural Teknology Foundation la kutoka nchini Kyenya, Merisent Sedi, alisema baada ya utafiti huo kukamilika watatoa elimu kwa wakulima ili wazalishe kitaalamu.

Alisema wakulima pia wataelekezwa kila mbegu namna ilivyo na manufaa ili wawe na uhuru wa kuchagua zile wanazoona zinawafaa kwenye kilimo chao.

"Lengo letu ni kuhakikisha wakulima wanazalisha zao hili kwa tija zaidi tofauti na sasa ambapo jua likiwaka kidogo tu wanaanza kuhaha, tunataka mtu akichukua mkopo kwa ajili ya kilimo asiwe na hofu ya kukosa mavuno kwa sababu ya kukosa mvua," alisema Sedi. Alisisitiza kuwa Wilaya ya Kyela ina maeneo mengi ambayo yanafaa kwa kilimo, lakini kutokana na kilimo cha eneo hilo kutegemea zaidi umwagiliaji hayalimwi na kwamba mbegu hizo zitakuwa suluhisho.

Aliwataka wataalamu wa kilimo katika maeneo mbalimbali kutembelea shamba hilo la utafiti ili wazitumia mbinu zilizotumika kuwaelimisha wananchi.



## SMZ yaahidi uongozi ujio Chuo cha Bima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameuhakikishia uongozi wa Chuo cha Bima na Hifadhi ya Jamii Afrika kuwa Serikali ya Zanzibar itaendelea kutoa ushirikiano wake katika kufanikisha azma ya kufungua chuo chao Zanzibar.

Hemed alieleza hayo juzi wakati akizungumza na viongozi wa chuo hicho waliofika ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha na kubadilishana naye mawazo.

Makamu wa Pili wa Rais aliupongeza uongozi wa chuo hicho, kwa kuwa na maono, ambayo yanadhihirisha uwezo mzuri waliokuwa nao katika kuisaidia jamii ya kitanzania.

Alisema ujio wa chuo hicho kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuitangaza Zanzibar sambamba na kutoa fursa kwa Wazanzibari kupata huduma mbalimbali ikiwamo fursa za ajira.

Naye Mwenyekiti Mtendaji wa Chuo cha Bima na Hifadhi ya Jamii Afrika, Dk. Baghayo Saqware, alisema kuwa, uongozi wa chuo hicho unakusudia kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha huduma za fedha, jambo, ambalo litasaidia kuunga mkono ajenda ya uchumi wa bluu.

Pia alieleza kwamba kitendo cha kuwa kitovu cha huduma za kifedha Zanzibar itafaidika kwa njia nyingi ikiwamo mikataba muhimu ya kimkakati sambamba na taasisi zingine za kifedha kuweka ofisi zao visiwani Zanzibar.

Dk. Saqware alisema Chuo cha Bima na Hifadhi ya Jamii Afrika kina maono yenye mrengo wa Kiafrika wa chuo cha kisasa kinachotoa mafunzo ya, utafiti, ushauri na ufumbuzi wa kimkakati katika maeneo ya bima, hifadhi ya jamii, masoko ya mitaji na uongozi katika sekta ya bima na fedha.

# Taasisi zinazokusudia kujenga majengo ya serikali zapewa neno

**Na Rahma Suleiman**,
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka taasisi zinapofikiria kuwa na miradi ya ujenzi wa majengo ya serikali kuwa na mtazamo wa kukidhi mahitaji makubwa ya sasa na baadaye.

Aliyasema hayo alipotembelea maonyesho ya ardhi, makazi na maendeleo ya ujenzi yaliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar.

Alisema majengo mengi ya serikali yanayojengwa kwa muda mfupi huwa hayakidhi na kutotosheleza mahitaji halisi kwa shughuli za serikali, kutokana na kuwepo fikra zisizozingatia mahitaji muhimu ya sasa na ya baadaye.

Alisema kuwepo ujenzi wa majengo yanayolenga mtazamo mkubwa wa sasa na baadaye ni jambo muhimu na inawezekana katika kuweka mipango bora ya maendeleo ambayo kwenye kipindi cha angalau miaka 50 ijayo kusifikiriwe ujenzi mpya.

Alisema kwa kuzingatia hali hiyo, ni vyema miradi ya ujenzi inayoanzishwa kuelekeza fikra katika majengo yenye ghorafa nyingi zaidi zitakazoweza kukidhi mahitaji makubwa yaliyopo na yajayo kwa kipindi kirefu.

Aidha, alishauri kwamba majengo ya serikali yanayoanzishwa pia ni vyema yakazingatia utamaduni halisi wa visiwa vya Zanzibar ili kutunza na kuendeleza kielelezo cha utamaduni wa Wazanzibari.

Hata hivyo, aliwapongeza waandaaji wa maonyesho hayo kwamba suala hilo ni muhimu kwa kuwasaidia wanajamii kuona mambo mbalimbali muhimu ya kimaendeleo yaliyopo katika nyanja hiyo.

Aidha, aliishauri Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kufikiria, kuwapunguzia mzigo wa kodi na tozo nyingi wananchi na wafanyabiashara wanapofanya miamala ya masuala ya nyumba na ardhi kwa kuwa tozo zilizopo sasa ni kubwa na zinawabebesha mzigo zaidi wananchi.

Alisema eneo hilo ni muhimu kuangaliwa na taasisi husika kwa kuwa linaweza kupunguza sana wananchi kufanya miamala ya namna hiyo kwa njia zisizo rasmi kwa kukimbia mzigo wa kodi na tozo mbali mbali zilizopo.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Makazi, Joseph John Kilangi, alimpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutembelea maonyesho hayo yaliyowapa fursa wananchi mbalimbali kuona kazi zilizoandaliwa na wadau tofauti.

Maonyesho hayo yalishirikisha taasisi mbalimbali zinazojishughulisha na masuala ya ujenzi, masuala mbalimbali ya aina hiyo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na uongozi wa Chuo cha Bima na Hifadhi ya Jamii Afrika waliofika ofisini kwake Vuga kujitambulisha na kubadilishana naye mawazo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vijana waonyeshwa fursa uchumi bluu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Makazi, Riziki Pembe Juma, amewataka vijana kuzitumia vizuri fursa za uchumi wa bluu ili kupata maendeleo.

Alisema Zanzibar imezungukwa na bahari, hivyo vijana wakizitumia vizuri rasilimali za bahari wataondokana na hali ya utegemezi.

Aliyasema hayo katika maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa Jumuiya ya Jukwaa la Vijana Zanzibar (ZYF), hafla ambayo ilifanyika Kariakoo Mjini Unguja.

Alisema vijana watakapozitumia rasilimali za bahari wataondokana na tatizo la ukosefu wa ajira ambapo kutokuwa na ajira kunawapelekea kujiingiza katika vitendo viovu ikiwamo utumiaji wa dawa za kulevya.

Waziri huyo aliwapongeza viongozi wa taasisi hiyo kwa kuwasaidia vijana wengi katika kutatua changamoto mbalimbali ikiwemo kuwapatia elimu vijana ya kuendelea kudumisha amani ya nchi.

“Vijana mna deni kubwa sana, hivyo tuendeleze kuyaenzi haya waliyoyaanzisha wenzetu na wameona umuhimu wa kuendeleza amani ya nchi, hivyo tuiendeleze,” alisema.

Aidha, aliwataka vijana kuendelea kutoa taaluma kwa vijana wenzao jinsi ya kujikinga na utumiaji wa dawa za kulevya sambamba na kuendelea kushajihishana na chanjo ya corona ili kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo.

“Nimefurahi sana kuona jumuiya hii hapa leo kutimiza miaka 20 hakika ni hatua nzuri sana wamefanya kazi kubwa kufika hapa, hii ni kutokana na matunda waliyoyaanzisha kwa vijana,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa ZYF, Fakih Kombo Faki, alisema, jumuiya hiyo imekuwa ikifanya kazi nyingi za kijamii ikiwamo kuwapatia vijana elimu juu ya mwendelezo wa kutunza amani katika nchi.

Alisema bila ya amani nchini, maendeleo hayatapatikana na vijana watapata matatizo mbalimbali ikiwamo kupoteza maisha na kupata majeraha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Jukwaa la Vijana Zanzibar Youth Forum (ZYF), Maulid Suleiman, alisema kuwa vijana wapo tayari kuona wanapigania mambo mbalimbali yanayotekelezwa na serikali na taasisi ili kupata maendeleo.

HABARI KIMATAIFA

# Waziri Mkuu Sudan kizuizini, yatangazwa hali ya hatari

**Khartoum, SUDAN**

KIONGOZI Mkuu wa kiraia na Waziri Mkuu, Abdallah Hamdok, ameripotiwa kuzuiliwa na wanajeshi, pamoja na mawaziri wengine kadhaa.

Inaonekana pia makao makuu ya televisheni na redio yamechukuliwa na jeshi huku mitandao ikifungwa.

Mkuu wa Baraza Kuu la Sudan, Abdel Fattah al-Burhan, ametangaza hali ya hatari, kuvunjwa kwa serikali ya mpito na Baraza la Mawaziri.

Jaribio la mapinduzi lililoshindwa mwezi uliopita lilizidisha mvutano.

Na katika wiki za hivi karibuni nchi hiyo imeshuhudia maandamano yakitaka jeshi lichukue madaraka pamoja na maandamano makubwa yanayomuunga mkono waziri mkuu.

Shirika la Haki za Binadamu, Human Rights Watch, lilisema jeshi kuchukua mamlaka Sudan ni pigo kubwa kuelekea utawala wa kiraia.

Sudan kwa sasa inaongozwa na baraza huru la pamoja la jeshi na raia.

Kundi la jeshi lilipangiwa kukabidhi uongozi kwa baraza huru la kiraia mwezi ujao.

Human Rights Watch lilisema jamii ya kimataifa inapaswa kushinikiza kurejea kwa kipindi cha mpito cha raia.

Shirika hilo lilivitaka vikosi vya usalama nchini humo kulinda haki za raia na kuacha kutumia mabavu.

Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Abdel Fattah Abdelrahman Burhan, alitarajiwa kuhutubia taifa huku waandamanaji wanaounga mkono jeshi wameishutumu serikali kwa kushindwa kufufua utajiri wa nchi hiyo wakati uhaba wa mkate ukikithiri.

Hatua ya Hamdok za kurekebisha uchumi pamoja na kupunguza ruzuku ya mafuta hazijapendwa na wengine.

Kulingana na ukurasa wa Facebook wa wizara ya habari, waziri mkuu sasa ametoa wito kwa watu kujitokeza kuunga mkono serikali.

Picha na ripoti zingine zinazotoka katika mji mkuu, Khartoum, zinaonyesha kwamba kuna waandamanaji nje ya jiji.

Wanajeshi pia wametumwa kuzuia usafiri wa watu kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Juni mwaka 2019, kabla ya mabadiliko ya kidemokrasia kukubaliwa, wanajeshi walifyatulia risasi waandamanaji huko Khartoum na kuua watu wasiopungua 87.

Kumbukumbu za mauaji hayo zitakuwa zikijirudia kwenye akili za watu wakati pande hizo mbili zikikabiliana.

Safari za ndege za kwenda na kutoka katika mji mkuu Khartoum zimesitishwa, huku kukiwa na taarifa za mapinduzi.

Watu wasiojulikana wenye silaha walikamata viongozi kadhaa wa Sudan nyumbani mwao jana asubuhi, baada ya mvutano wa wiki kadhaa kati ya jeshi na mamlaka ya raia katika nchi hii ya Afrika Mashariki.

Serikali ya mpito iliyoundwa kati ya raia na Baraza la kijeshi, mwaka 2019 baada ya kuangushwa kwa utawala wa kiongozi wa muda mlrefu Omar Al Bashir kufuatia maandamano ya wananchi, na ilipaswa kuongoza mpaka mwaka 2023 na kupisha uchaguzi mkuu, imefutwa.

**BBC**



Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Abdel Fattah Abdelrahman Burhan. **PICHA: BBC**

# Familia yaukataa mwili mshukiwa mauaji

**Nairobi, KENYA**

FAMILIA ya mshukiwa sugu wa mauaji ya watoto aliyekiri ambaye aliuliwa kwao baada ya kutoroka kutoka mahabusu ya polisi imemkana.

Familia ya Masten Wanjala imesema haitamzika kwa sababu inahofia kupata laana.

Familia hiyo iliamua hata kukwepa kushiriki uchunguzi wa mwili wa mtoto wao kwa njia ya DNA uliofanywa na maofisa wa uchunguzi wa mwili kwa kuogopa laana.

Naibu Chifu wa MukhweyaAbiud Musungu alisema kuwa familia ya Wanjala ilikataa kupokea simu kutoka kwa maofisa ili wachukuliwe vipimo vya vinasaba-DNA na kumzika mtoto wao huyo wa kiume.

Chifu huyo alisema huenda serikali ikalazimika kumuua mshukiwa huyo wa mauaji iwapo familia itaendelea kuwa na msimamo wa kumkana.

Jirani wa Wanjala, Davis Wafula, alisema kuwa kama ukoo hawakutaka kujihusisha naye kwa sababu aliwaaibisha.

"Tunaogopa iwapo tutamzika, sisi, kama ukoo, tunaweza kuonekana kama wauaji," alinukuliwa na vyombo vya habari, Wafula, akisema.

Masten Wanjala, aliyekuwa na umri wa miaka 20, alipatikana katika nyumba iliyopo katika mji wa Bungoma magharibi mwa nchi hiyo, baada ya kutoroka mahabusu ya polisi Nairobi na kupigwa hadi kufa na wanakijiji wenye hasira.

Kabla ya kifo chake Hasten Wanjala alikiri binafsi kuwaua watoto 10 katika kipindi cha miaka mitano.

Pia alikiri kuwavuta na wakati mwingine hata kunywa damu yao.

Aliripotiwa kurudi katika nyumba ya wazazi wake ambao walikuwa tayari wamemkataa na hatimaye alipigwa na kunyongwa na majirani ambao walibaini kuwa alikuwa pale, zilisema taarifa za vyombo vya habari nchini Kenya.

**BBC**

## Kundi IS ladai kuhusika shambulio bomu Kampala

**Kampala, UGANDA**

KUNDI linalojiita Dola la Kiislamu, IS limedai kuhusika na shambulizi la bomu lililoua mtu mmoja katika mji mkuu wa Kampala Jumamosi usiku, mwishoni mwa wiki.

Hayo yameelezwa kupitia ukurasa wa mtandao wa Telegram wenye mafungamano na kundi hilo.

IS ilisema baadhi ya wanachama wake wamelipua bomu hilo katika kilabu ambacho hupendelewa na majasusi wa serikali ya Uganda, ambayo kundi hilo limeitaja kuwa adui wa Uislamu.

Taarifa ya polisi wa Uganda, juzi, ilisema kuwa shambulio hilo liliilenga baa inayouza nyama ya nguruwe katika kitongoji kimoja cha mji wa Kampala.

Ilisema wanaume watatu waliingia kama wateja katika baa hiyo, wakaweka mfuko wa plastiki wenye viripuzi chini ya meza moja, na wakaweza kutokomea kabla ya mlipuko kutokea.

Rais wa Uganda Yoweri Museveni (pichani), alisema shambulio hilo linaonekana kuwa la kigaidi.

Mbali na mmoja aliyeuawa katika shambulio hilo, liliwajeruhi wengine watatu, wawili wakiwa katika hali mahututi.

**DW**



**Ilisema wanaume watatu waliingia kama wateja katika baa hiyo, wakaweka mfuko wa plastiki wenye vilipuzi chini ya meza moja, na wakaweza kutokomea kabla ya mlipuko kutokea.**

# GALAXY YASEMA DHARAU CHANZO KIPIGO SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Jwaneng Galaxy ya Botswana aliyefunga mabao mawili kwenye mechi dhidi ya Simba, Rudath Wendell, amesema wapinzani wao walidharau na kuamini tayari wamepita, na wao wakatumia mwanya huo kuwaangamiza.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Simba ikifungwa mabao 3-1 na kutolewa kwenye michuano hiyo kwa faida ya bao la ugenini, matokeo ya jumla yakiwa ni 3-3, kutokana na Simba kushinda 2-0 ugenini, mchezaji huyo alisema anamshukuru Mungu kwa kuisaidia timu yake kusonga mbele na aliamini kuwa anaweza kufunga bao, baada ya kuingia kipindi cha pili akitokea benchi.

"Namshukuru Mungu kwa kufunga mabao haya, naweza kusema ni kuamini kwamba chochote kinaweza kutokea, niliamini kwamba nitafunga nikiingia. Simba siyo timu mbaya, ni timu nzuri sana sana, na ilitawala kipindi cha kwanza.

"Kocha wetu alituambia tusihofia kitu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na akaniingiza nikaenda kubadili matokeo," alisema mchezaji huyo aliyefunga mabao hayo sekunde chache tu baada ya kuanza kwa kipindi cha pili, na dakika ya 59.

Aliongeza kuwa wachezaji wa Simba waliamini wamemaliza kazi, baada ya kupata bao moja, huku wakiwa na mtaji wa mabao mawili ugenini.

"Walitudharau, waliamini kuwa tayari wamemaliza kazi, lakini sisi tuliamua kupambana hadi dakika za mwisho kama kocha wetu alivyotuambia," alisema.

Simba imetolewa kwenye michuano hiyo na kuangulia Kombe la Shirikisho Afrika, na sasa inasubiri droo kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kujua itapangiwa na timu gani kwenye hatua ya mtoano, kabla ya kutinga makundi.

## WAREMBO...




Meneja Uzalishaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti kiwanda cha Mwanza, RoLinda Samson (wa kwanza kulia) akizungumza na warembo wanaoshiriki shindano la Miss Kanda ya Ziwa waliotembelea kiwanda hicho jana. Kulia kwake ni Meneja Mauzo wa SBL, Patrick Kisaka. Shindano hilo linadhaminiwa na Bia ya Pilsner Lager inayotengenezwa na kiwanda hicho. **MPIGAPICHA WETU**

# Harerimana apania 3 za Biashara United

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya Kwanza FC, Haruna Harerimana, amesema wanamejiandaa vizuri kuelekea mchezo wao dhidi ya Biashara United na wako tayari kupambana kutafuta ushindi katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbeya Kwanza itaikaribisha Biashara United Ijumaa wiki hii katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya. Akizungumza na gazeti hili jana, Hererimana alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo wa wanne kwao wa Ligi Kuu ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwa kubakiza pointi tatu nyumbani kutoka kwa Biashara United.

Alisema ana tambua mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wapinzani wao wametoka katika michuano ya kimataifa hivyo watakuwa bora, lakini wao ni bora zaidi yao.

"Tunahitaji kwanza matokeo mazuri ikiwamo kutumia vema uwanja wetu wa nyumbani na kutafuta ushindi wetu wa pili katika mchezo yetu minne. Tunakwenda kucheza dhidi ya Biashara United, kikubwa pointi tatu idadi ya mabao tunamuachia Mungu," alisema Harerimana.

Kwa upande wa wachezaji wake, alisema wote wako fiti na anaimani watapata matokeo mazuri kwa sababu ya morali wao wa kuhitaji ushindi kuwa juu.

Hadi sasa Mbeya Kwanza FC wameshinda mechi moja dhidi ya Mtibwa Sugar, sare mbili dhidi ya Namungo FC na Mbeya City, hivyo kujikusanyia pointi tano kwenye msimamo wa ligi hiyo, unaongozwa na Polisi Tanzania walipo kileleni wakiwa na alama tisa sawa na Yanga inayozidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

## Makata aipigia hesabu Mtibwa

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 juzi, Kocha Mkuu wa Klabu ya Dodoma Jiji, Mbwana Makata, amesema mchezo wao dhidi ya Tanzania Prisons, ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka jijini Dodoma, Makata alipongeza wachezaji wake kwa kutumia nafasi walizozipata mpaka kupata ushindi huo kwenye mechi hiyo iliyopigwa usiku kwa mara ya kwanza katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

"Ninashukuru jana [juzi] usiku tulimaliza mchezo tukiwa na ushindi wa mabao mawili, sasa hivi ninajipanga kwa ajili ya kukutana na timu ya Mtibwa Sugar," alisema Makata.

Kocha huyo alisema kuwa jana aliwapumzisha wachezaji wake kabla ya kuendelea na mazoezi leo asubuhi kujiandaa na mechi dhidi ya Mtibwa Sugar ugenini Jumamosi wiki hii.

## Mbunge kupeleka wachezaji Qatar

**Na Tumaini Mafie, Monduli**

MBUNGE wa Monduli, Fred Lowasa, ametoa ahadi ya kuwapeleka wachezaji bora watakaofanya vizuri katika michezo yao ya mashindano ya Kombe la Fred Lowasa, kuangalia Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani.

Lowasa alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa halfa ya uzinduzi wa mashindano hayo, uliofanyika Kata ya Meserani wilayani Monduli, Arusha.

"Mashindano haya yatafanyika kila mwaka na nimetoa ahadi yangu kwa kuwapeleka kuangalia Kombe la Dunia mchezaji bora, mchezaji mwenye nidhamu na mfungaji bora, wote nitawapeleka kwenda kuangalia Kombe la Dunia na watasindikizwa na wazazi wao. Hivyo naombeni sana mjitahidi kuonyesha vipaji vyenu mkiwa bado wadogo kwani hayo ndiyo maandalizi ya kuwa wachezaji maarufu kama walivyo wengine," alisema Fred.

Fred alisema kuwa, amefikia hatua ya kuzisaidia timu hizo kwa lengo la kuinua vipaji kwa watoto waliopo chini ya miaka 15, huku lengo likiwa ni kuhakikisha wanatoa mchezaji bora kutoka Wilaya ya Monduli ili watoto hao waweze kuwa na moyo wa kuipenda michezo tangu wakiwa wadogo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MARCELO KUONDOKA MADRID

MLINZI wa kushoto wa Brazili, Marcelo mwenye umri wa miaka 33, ameiambia Real Madrid kwamba ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu na huenda akatua klabu ya Fluminese ya nyumbani kwao, Brazil. **(El Nacional)**

### PERISIC AWANIWA EVERTON

EVERTON na West Ham ni miongoni mwa klabu zinazomwania winga wa Inter Milan, Ivan Perisic mwenye umri wa miaka 32. Hata hivyo, klabu za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, zimeonyesha pia nia za kumtaka Mcroatia huyo. **(Fichajes)**

### HAG ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United itapaswa kuweka mezani ofa ya kipekee na isiyo ya kawaida kumpata bosi wa Ajax, Erik ten Hag ili kuinoa timu hiyo. **(Chronicle Live)**

### FULGINI AWINDWA EPL

KIUNGO wa Angers, Angelo Fulgini, anazivutia klabu za Ligi Kuu England (EPL), baada ya Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 25 kufunga bao dhidi ya Paris St-Germain mwishoni mwa juma lililopita. **(Sun)**

### RICE DAU NENE SOKONI

KOCHA wa West Ham, David Moyes, ameonya kwamba klabu yoyote inapaswa kulipa kitita kinene cha zaidi ya pauni milioni 100 ili kumsajili kiungo wa England, Declan Rice. **(Sky Sports via Manchester Evening News)**

### CHELSEA YAMUULIZIA DIAZ

CHELSEA imeulizia kuhusu upatikanaji wa winga wa Porto, Luis Diaz, lakini klabu za Newcastle, Bayern Munich na Real Madrid pia zimewasiliana na wawakilishi wa winga huyo mwenye miaka 24. **(Nicolo Schira on Twitter)**

### NDOMBELE ATOA LA MOYONI

KIUNGO Mfaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 24, amesema kikao chake na Mwenyekiti wa klabu hiyo, Daniel Levy, kiliokoa maisha yake ya soka pale Tottenham Hotspurs. **(Sun)**

### RUDIGER KUONDOKA CHELSEA

MLINZI wa kati wa Chelsea, Antonio Rudiger, anatajwa kutaka kuondoka Stamford Bridge msimu ujao, huku Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 28, akihusishwa na klabu za Juventus, Manchester City, Tottenham na Paris St-Germain. **(Wettfreunde)**

### POGBA HAKIJAELEWEKA

MAZUNGUMZO kati ya Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28 na Manchester United kuhusu Mfaransa huyo kusaini mkataba mpya, yamesimamishwa na wakala wake, Mino Raiola hadi Aprili mwakani. **(AS)**

### KASSIE, MILAN SASA POA

AC Milan na kiungo, Franck Kassie mwenye umri wa miaka 24, wamefikia mahali pazuri kuhusu mkataba mpya wa nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, huku akihuishwa na kutakiwa na klabu kadhaa Ulaya. **(Calcio Mercato)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH SASA MFUNGAJI BORA WA AFRIKA EPL

●●●Ampiku Drogba, pia amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick Uwanja wa Old Trafford katika...

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah, amekuwa mchezaji wa kwanza wa Afrika kufunga mabao mengi zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu England, baada ya 'hat trick' yake dhidi ya Manchester United pale Old Trafford, Jumapili.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri sasa amemzidi mshambuliaji wa zamani wa Chelsea, Didier Drogba mwenye mabao 104, huku yeye akifikisha mabao 107 kwenye ligi hiyo.

Kwanza alifunga dakika ya 38 akifikisha idadi sawa ya mabao na Drogba, kabla ya kumzidi wakati alipofunga la nne kabla ya mapumziko na kuifanya timu yake kuwa mbele kwa 4-0.

Alifunga bao la tano dakika ya 50, na kufanya hivyo, kumemfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick kwenye Uwanja wa Old Trafford katika historia ya Ligi Kuu England.

Drogba alifunga mabao hayo 104 wakati akicheza pale Chelsea katika vipindi viwili tofauti kabla ya kuondoka mwaka 2015.

Na sasa Salah mwenye umri wa miaka 29, anakuwa mchezaji wa kwanza wa Afrika kufunga mabao 106 kwenye ligi hiyo.

Salah awali alifunga bao moja katika mechi 13 alizocheza kule Chelsea mwaka 2014, lakini mengine yote ameyapata wakati akicheza pale Liverpool ambako alisajiliwa mwaka 2017.

Alishinda Kiatu cha Dhahabu kama mfungaji bora msimu wa 2017-18, huku pia Salah aliisaidia Liverpool kushinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu England kwa kipindi cha miaka 30, msimu wa 2019-20.

Drogba, ambaye alicheza katika vipindi viwili tofauti pale Chelsea kutoka mwaka 2004 hadi 2012 na msimu wa 2014-15, alishinda Kiatu cha Dhahabu mara mbili katika vipindi viwili (2006-07 na 2009-10) na alishinda taji la Ligi Kuu mara nne.

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 619

MECHI KALI
HOME AWAY
CHELSEA
1.44 | 4.35 | 6.73
SOUTHAMPTON

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BARCA YALAANI GARI LA KOEMAN KUSHAMBULIWA



**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imelaani kitendo cha mashabiki kuvamia gari la kocha Ronald Koeman wakati anaondoka kwenye Uwanja wa Camp Nou baada ya kufungwa mabao 2-1 na Real Madrid katika mchezo wa kwanza wa Clasico wa msimu huu, Jumapili.

Mabao kutoka kwa David Alaba na Lucas Vazquez yaliiweka Madrid kwenye uongozi na Sergio Aguero alifunga la kufutia machozi dakika ya mwisho, wakati Barca wakifungwa kwa mara ya nne mfululizo mchezo wa Clasico mara tatu ikiwa chini ya Koeman.

Raia huyo wa Uholanzi ni kocha wa pili katika historia ya Barca kufungwa mechi tatu za LaLiga na Real Madrid, baada ya Patrick O'Connell aliyekumbana na kadhia hiyo mwaka 1935 na 1940.

Wakati Barca ikiwa nafasi ya tisa kwenye msimamo wa LaLiga na ya tatu kwenye kundi la Ligi ya Mabingwa Ulaya, presha inadizi kuwa kubwa kwa Koeman wakati mashabiki wakiwa hawaridhishwi na kiwango cha timu.

Na hiyo ikajitokeza Jumapili baada ya kupoteza kwa 'Los Blancos', kundi la mashabiki lilivamia gari la Koeman wakati linaondoka uwanjani hapo.

Barca ilitoa taarifa kulaani kitendo hicho cha mashabiki na kusema wataongeza ulinzi ili tukio hilo lisijirudie tena.

"FC Barcelona inalaani hadharani fujo alizofanyiwa kocha wetu wakati anaondoka Uwanja wa Camp Nou," ilisomeka taarifa hiyo.

"Klabu itaongeza ulinzi na kuchukua hatua za kinidhamu kwa tukio kama hilo na inaamini halitajitokeza tena."

# Lukaku ashutumiwa kupenda fedha



**MILNA, Italia**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Inter Milan, Beppe Marotta, ametoa povu kwa mshambuliaji wa zamani wa klabu hiyo aliyejiunga na Chelsea, Romelu Lukaku kwa kusema amekimbilia huko ili kuongeza mshahara wake.

Lukaku alijiunga na Chelsea kwa ada ya pauni milioni 98 kipindi cha majira ya joto huku akidai hawajutii kuachana na mshambuliaji huyo na kumsajili Edin Dzeko kuziba pengo lake.

"Lukaku ameuzwa kwa euro milioni 115 na tumemleta Edin Dzeko bure. Uwanjani hakuna tofauti kubwa," alisema Morotta akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Lukaku aliondoka ili kuongeza mshahara wake, Italia namba hizo hazipo," aliongeza Marotta.

"Leo hatuwezi kuweka uwekezaji muhimu, sikuweza kuruhusiwa kumsajili Lukaku kwa euro milioni 70. Tunahitaji kupunguza na uwekezaji maalum."

Lukaku alifunga mabao 64 katika mechi 95 alizocheza akiwa Inter Milan kabla ya baadaye kuamua kurejea katika klabu yake ya zamani ya Chelsea.

## HABARI MICHEZO


,207,580

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/10/21 | 17:00 | Watford vs Southampton | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 02. 30/10/21 | 17:00 | Burnley vs Brentford | 2.80 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 30/10/21 | 17:00 | Derby vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 04. 30/10/21 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 05. 30/10/21 | 18:00 | Metz vs St Etienne | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 06. 30/10/21 | 19:30 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.79 | 3.38 | 2.49 |
| 07. 30/10/21 | 19:30 | Valencia vs Villarreal | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 31/10/21 | 15:00 | Angers vs Nice | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 31/10/21 | 16:00 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.67 | 2.97 | 2.92 |
| 10. 31/10/21 | 17:00 | Bordeaux vs Reims | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 11. 31/10/21 | 17:30 | Augsburg vs Stuttgart | 2.80 | 3.30 | 2.47 |
| 12. 31/10/21 | 19:30 | Aston Villa vs West Ham | 2.77 | 3.42 | 2.49 |
| 13. 31/10/21 | 22:45 | Roma vs AC Milan | 2.49 | 3.42 | 2.77 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 26 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5026 | KS Lechia Zielona Gora vs Arka Gdynia | 8.89 | 5.03 | 1.28 |
| 15:00 | 2048 | Lokomotive Sofia vs Lokomotiv Plovdiv | 2.65 | 3.13 | 2.51 |
| 15:00 | 3168 | Acso Filiasi vs Hermanstadt | 5.22 | 3.82 | 1.56 |
| 15:00 | 5625 | Gazovik Orenburg vs Dinamo Moscow | 7.15 | 4.06 | 1.41 |
| 16:00 | 5101 | NK Belisce vs Hajduk Split | 21.00 | 9.00 | 1.11 |
| 17:00 | 5822 | Cobresal vs O Higgins | 1.66 | 3.63 | 4.65 |
| 17:20 | 3809 | Umm-Salal SC vs Al Sadd SC | 13.52 | 7.34 | 1.13 |
| 17:20 | 5845 | Al Rayyan SC vs Al-Sailiya SC | 1.50 | 4.15 | 5.40 |
| 17:55 | 3009 | AL Kawkab vs Bisha FC | 2.35 | 3.04 | 2.94 |
| 18:05 | 2055 | AL Khlood vs Al Wehda | 5.61 | 3.58 | 1.57 |
| 18:30 | 1318 | El Gouna vs Ceramica Cleopatra | 3.45 | 3.05 | 2.19 |
| 18:30 | 1832 | HNK Sibenik vs Slaven Belupo | 2.25 | 3.35 | 3.15 |
| 18:30 | 4638 | Bohemians vs Jihlava | 1.41 | 4.17 | 6.98 |
| 19:00 | 4443 | Horsens vs Vejle BK | 2.47 | 3.43 | 2.51 |
| 19:30 | 1279 | Hoffenheim vs Holstein Kiel | 1.40 | 5.19 | 6.59 |
| 19:30 | 1868 | 1860 Munich vs Schalke 04 | 3.51 | 3.66 | 1.99 |
| 19:30 | 2263 | Venezia vs Salernitana | 2.08 | 3.36 | 3.62 |
| 19:30 | 2572 | Spezia vs Genoa | 2.50 | 3.41 | 2.76 |
| 19:45 | 3269 | Stedoco vs Utrecht | 17.47 | 7.96 | 1.10 |
| 20:00 | 2561 | Alaves vs Elche | 2.32 | 3.02 | 3.42 |
| 20:00 | 3271 | Helsingborg vs Gais | 1.75 | 3.70 | 4.60 |
| 20:00 | 4347 | Avranches vs Annecy FC | 3.32 | 3.42 | 2.03 |
| 20:00 | 5279 | Trelleborgs FF vs AFC Eskilstuna | 1.92 | 3.61 | 3.81 |
| 20:00 | 5783 | Bourg Peronnas vs Concarneau | 1.77 | 3.42 | 4.40 |
| 20:15 | 3529 | Ittihad Tanger vs Mouloudia Oujda | 2.76 | 2.71 | 2.76 |
| 21:00 | 1410 | Kozakken Boys vs Telstar | 3.40 | 3.83 | 1.85 |
| 21:00 | 1487 | Zamalek vs Enppi Club | 1.31 | 5.14 | 8.71 |
| 21:00 | 1727 | PEC Zwolle vs De Graafschap | 2.32 | 3.33 | 2.75 |
| 21:00 | 3290 | Borussia Dortmund vs Ingolstadt | 1.12 | 8.40 | 20.99 |
| 21:00 | 3442 | Dinamo Bucuresti vs Argesul Pitesti | 2.71 | 3.05 | 2.51 |
| 21:00 | 4707 | Roda Kerkrade vs Den Bosch | 1.50 | 4.35 | 5.03 |
| 21:30 | 2126 | Mechelen vs Union Saint Gilloise | 3.16 | 3.70 | 2.01 |
| 21:30 | 3845 | Morton vs Partick Thisle | 3.08 | 3.38 | 2.15 |
| 21:45 | 1472 | Notts County vs Bromley | 1.98 | 3.52 | 3.37 |
| 21:45 | 1817 | Hamilton vs Queen of South | 2.32 | 3.38 | 2.79 |
| 21:45 | 1841 | Mouscron Peruwelz vs Standard Liege | 3.77 | 3.92 | 1.77 |
| 21:45 | 1918 | Chelsea vs Southampton | 1.44 | 4.35 | 6.73 |
| 21:45 | 2621 | Colchester vs Sutton United | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 21:45 | 2659 | Mainz vs Arminia Bielefeld | 1.67 | 3.94 | 4.79 |
| 21:45 | 3541 | AC Milan vs Torino | 1.59 | 4.13 | 5.44 |
| 21:45 | 3805 | Arsenal vs Leeds | 1.66 | 3.76 | 4.88 |
| 21:45 | 4647 | QPR vs Sunderland | 1.93 | 3.64 | 3.54 |
| 21:45 | 5230 | Nurnberg vs Hamburger SV | 2.81 | 3.41 | 2.44 |
| 21:45 | 5362 | Wigan vs Lincoln | 1.73 | 3.85 | 4.24 |
| 21:45 | 5548 | Dunfermline vs Raith Rovers | 2.78 | 3.36 | 2.34 |
| 21:45 | 5690 | Doncaster vs Cambridge Utd | 2.32 | 3.27 | 2.97 |
| 21:45 | 5710 | Osnabruck vs SC Freiburg | 5.79 | 4.39 | 1.52 |
| 21:45 | 5861 | Inverness vs Arbroath | 1.90 | 3.60 | 3.56 |
| 22:00 | 3320 | Espanyol vs Athletic Bilbao | 2.80 | 3.00 | 2.75 |
| 22:30 | 2822 | Villarreal vs Cadiz CF | 1.42 | 4.63 | 7.45 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# RONALDO AWAONEA HURUMA MASHABIKI UTD




**MANCHESTER, England**

CRISTIANO Ronaldo amesema mashabiki wa Manchester United "wanastahili kitu bora" baada ya Jumapili kukumbana na kichapo cha unyanyasaji cha mabao 5-0 kwenye Ligi Kuu England kutoka kwa Liverpool.

Ilikuwa siku isiyosahaulika kwa Ronaldo na United, ambao walinyanyaswa kwenye Uwanja wa Old Trafford, ambapo 'Mashetani Wekundu' hao walijikuta wakitandikwa mabao manne katika kipindi cha kwanza, kabla ya Paul Pogba kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

Mohamed Salah alifunga hat-trick wakati United wakiweka historia ya kuruhusu mabao matano au zaidi nyumbani bila wao kupata bao kwa mara ya kwanza tangu walipotandikwa 5-0 na Manchester City mwaka 1955.

United imefungwa mabao mengi zaidi na Liverpool kwa mara ya kwanza tangu Oktoba 1895 wakati walipofungwa 7-1 pale kwenye Uwanja wa Anfield, huku kikiwa kipigo kikubwa zaidi kuchapwa kwenye ardhi ya dimba lao.

Ronaldo, ambaye alionekana kuchanganyikiwa katika kipindi chote cha mchezo, alitumia mtandao wa kijamii kuelezea kile kinachoendelea ndani ya Manchester.

"Wakati mwingine matokeo yanakuwa si yale unayoyapigania. Muda mwingine matokeo si yale unayoyataka," aliandika mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Na hili ni suala letu sisi, ni sisi tu, kwa sababu hakuna wa kumlaumu kuhusu yale yanayotokea.

"Mashabiki wetu walikuwapo, kwa mara nyingine walitupa sapoti tunayoihitaji. Wanastahili kitu bora kuliko hiki, na ni suala letu kuweza kuimarika."

# Pochettino akunwa kiwango cha Neymar

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino ameelezea mwenyewe "nimeridhika" na kile alichokiona kwa Neymar wakati vinara hao wa Ligue 1 wakitoka suluhu na wapinzani wao, Marseille kwenye mchezo maarufu kama 'Le Classique'.

Neymar alirudi kwenye kikosi hicho baada ya kuikosa PSG ikishinda dhidi ya RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne akisumbuliwa na maumivu ya nyonga na alianza pamoja na Kylian Mbappe na Lionel Messi, Jumapili.

Umoja wao haukuwa na athari yoyote kwenye kikosi hicho, wakati safu hiyo ya ushambuliaji haikutengeneza mashambulizi ya maana dhidi ya Marseille pale kwenye Uwanja wa Velodrome.




PSG walilazimika kucheza wakiwa na wachezaji 10 uwanja kuanzia dakika ya 57, wakati mlinzi wa pembeni, Achraf Hakimi alipotolewa nje kwa kadi nyekundu.

Hilo likamfanya Neymar kurudi kwenye dimba la kati baada ya Thilo Kehrer kuchukua nafasi ya Angel Di Maria.

Neymar alitolewa nje dakika ya 83 na Georginio Wijnaldum akachukua nafasi yake.

Ilikuwa ni mara ya kwanza sare ya bila kufungana kati ya Marseille na PSG katika Uwanja wa Velodrome kwenye Ligue 1 tangu Novemba 1998.

"Baada kupoteza mchezaji mmoja, kulihitajika badiliko na tukafikiri kumwingiza Kehrer na kumrudisha Neymar kwenye safu ya kiungo," alisema Pochettino akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

Aliongeza: "Nimeridhishwa na mchezo aliouonyesha Neymar, alijitolea kwa ajili ya timu baada ya kurudi kutoka timu ya Tifa ya Brazil na amekuwa bora kabisa."

# Michezo

Jumanne Oktoba 26, 2021

Nipashe




Salah sasa mfungaji bora wa Afrika EPL

UKURASA 21

**WAPO SANA TU!...**




Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes (kushoto), akijadili jambo na wasaidizi wake, Selemani Matola (katikati) na Thierry Hitimana, makocha hao jana walidaiwa kukalia kuti kavu kutokana na kipigo dhidi ya Jwaneng Galaxy, lakini Nipashe lilipotaka ukweli kutoka kwa uongozi wa klabu hiyo, ulikanusha. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA SC YAGEUKIA WASALITI MECHI CAF

Kipigo Jwaneng Galaxy sasa kuondoka na mtu, ni baada ya jana vigogo wa klabu hiyo kujifungia kujadili wahusika...

**Na Saada Akida**

KIPIGO cha mabao 3-1 kutoka kwa Jwaneng Galaxy, ambacho kimesababisha Simba kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na kuangukia Kombe la Shirikisho Afrika, hakiwezi kuacha mtu salama ndani ya klabu hiyo, imeelezwa.

Simba ambayo mchezo wa ugenini ilishinda 2-0, hivyo kuhitaji ushindi ama sare yoyote au kutokukubali kufungwa zaidi ya mabao 2-0, ili kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo, juzi ilijikuta ikikubali kipigo cha mabao 3-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 3-3 na kutopwa nje kwa faida ya bao la ugenini.

Hata hivyo baada tu ya mchezo huo kumalizika, hali ya hewa ilichafuka kupitia kwa vigogo wa timu hiyo kutokana na kudai kubaini kulikuwa na usaliti wa hali ya juu uliochangia matokeo hayo.

Crescentius Magori ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba na Mshauri wa Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji, baada ya matokeo hayo alisema hii ni siku yenye giza 'nene' katika historia ya Simba.

"This is the darkest day in Simba history! [hii ni siku ya giza 'nene' katika historia ya Simba]," aliandika Magori katika mtandao wake wa twitter na kuongeza "Usaliti ni kitu kibaya sana, hakivumiliki!"

Kwa upande wa Mo Dewji, yeye aliandika: "Kwa kuwa tayari nimejiuzulu, siwezi kutoa maamuzi yoyote, lakini namshauri mwenyekiti na bodi yake wachukue hatua za haraka kwa waliochangia kipigo cha leo. Haikubaliki".

Lakini Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo (CEO), Barbara Gonzalez, yeye aliandika: "Leo tumejifunza somo: Kamwe usiwadharau wapinzani wako hadi filimbi ya mwisho itakapopulizwa. Hakuna dhamana katika mpira wa miguu, bado ninaamini tuna timu nzuri. Kuteleza si kuanguka, tutarudi tukiwa na nguvu zaidi".

Hata hivyo, jana vigogo wa timu hiyo walijifungia katika kikao chao cha ndani na ilielezwa walikuwa wakijadili adhabu ya kuwachukulia wahusika waliowabaini kufanya usaliti huo.

"Nina uhakika kwa zaidi ya asilimia 100 kuhusu usaliti uliofanywa, ila siwezi kukuambia lolote hadi kikao kimalizike na kutoa uamuzi, kwa kile kilichotokea," alisema mmoja wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, Nipashe lilipotaka kujua watuhumiwa wa usaliti huo.

Wakati huo huo, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, amesema hakutarajia matokeo hayo kutokana na maandalizi waliyofanya, lakini wao kama benchi la ufundi hawana wa kumtupia lawama na sasa wanajipanga kwa ajili ya Kombe la Shirikisho.

Alisema mipango yao, kwa sasa ni michezo ya Ligi Kuu Bara pamoja na hatua ya mtoano ya Kombe la Shirikisho ambayo wanasubiri wapangiwe moja kati ya timu zilizovuka raundi ya kwanza ya michuano hiyo zilizokuwa zikishiriki Kombe la Shirikisho.

"Hayakuwa matokeo mazuri kwetu nachukua nafasi hii kuwaomba radhi mashabiki wetu kwa matokeo haya, hakuna aliyetarajia mipango yetu ilikuwa kuingia hatua ya makundi lakini tumeshindwa kuendelea," alisema.

## Yanga yashushwa, Simba SC yaonywa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting juzi kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani, timu ya Polisi Tanzania imeishusha Yanga kileleni, huku ikiionya Simba kuwa itapata wakati mgumu katika mechi dhidi yao watakapokutana Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho.

Polisi Tanzania, baada ya kushinda mechi hiyo, sasa inaongoza ligi ikiwa na pointi tisa kama Yanga, lakini yenyewe inaidadi kubwa ya mabao ya kufunga.

Wakati Yanga ina mabao manne huku ikiwa hajaruhusu bao, Polisi Tanzania imefunga mabao matano, lakini imeruhusu bao moja.

Huu ni ushindi wa tatu mfululizo kwa timu hiyo msimu huu, ikianza kwa kuichapa KMC mabao 2-0, kabla ya kuifunga Azam FC mabao 2-1, mechi zote ikicheza nyumbani, kabla ya kushinda 1-0 ugenini dhidi ya Ruvu Shooting, likiwekwa wavuni na straika wake iliyomsajili msimu huu, Vitalis Mayanga, ambaye tayari amefikisha mabao matatu na kuongoza katika orodha ya wafungaji mpaka sasa.

Baada ya ushindi huo, klabu hiyo imeandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuwa kituo kinachofuata sasa ni Uwanja wa Benjamin Mkapa kuongeza machungu kwa wanachama na mashabiki wa Simba na hii ni baada ya kufungwa mabao 3-1, na kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ni wakati wa kuendeleza mapambano tuliyoyaanza. Pira chukuchuku litaonyeshwa na vijana wa Polisi Tanzania Jumatano, nyama ya simba inafaa sana ikipikwa chukuchuku, kila mmoja ataweza kuitumia. Nyote mnakaribishwa," Klabu ya Polisi Tanzania, iliandika kwenye mtandao wake wa kijamii.


9 770856 541002 >